

UWEPO WA MUNGU

USIOTAMBULIWA

 Sasa wakati umati wetu ukiwa ni mdogo, tunaenda kujaribu ku—kuharakisha, tutoke ili tuweze, tukifanya kazi kwa kusudi hili moja, ili mpate kuutambua Uwepo wa Yesu Kristo. Mnaona? Kama Yeye yupo, basi, mbona, kila kitu kimetatuliwa. Yeye alilileta Neno. Yupo hapa kulihakikisha. Yeye anathibitisha kwamba atalihakikisha. “Ni yeye yule tu jana, leo, na hata milele.” Tulimwona akilifanya jana usiku, pasipo kukosea; tunamwona, usiku baada ya usiku, na siku baada ya siku, na mwaka baada ya mwaka. Hakuna hata wakati mmoja Yeye amebashiri chochote, haidhuru ilikuwa ni lini, wakati gani lingetukia, katika maelfu ya nyakati, ya yale yaliyokuwa makamilifu kabisa, pasipo kuchelewa, na sahihi. Inawezekana? Ni wangapi wanaojua hilo, na wanajua huduma hii, na wanajua kwamba hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Haya basi. Si hata wakati mmoja, haidhuru, jinsi hata isivyowezekana, lilitukia vivyo hivyo. Yeye ni Mungu! Na kama tungalitambua tu jambo hilo, tulishike!

² Na sasa tuna wakati mfupi tu wa kuwa hapa. Nafikiri siku tatu zaidi usiku, ama siku mbili zaidi usiku na mchana, baada ya usiku wa leo. Nafikiri Jumapili alasiri ndiyo ibada ya kumalizia. Tunajitahidi kufunga Jumapili alasiri ili wachungaji na kila mtu... Hatutaki kuwazuia kwenda kanisani kwenu. Tunataka tu kuongezea wengi zaidi kanisani, na kuwapa imani zaidi katika Mungu mnyemtumikia kanisani mwenu. Mnaona? Wala hatutaki milango ya kanisa ifungwe, kwa vyovyote vile. Tunawatakeni mkae mle, bali tunajaribu tu kuwasaidia, kuwapa moyo. Uamsho hata haumaanishi kuongeza wengi zaidi kanisani; uamsho unamaanisha kuwahuisha wale mlilo nao tayari; hiyo ni kweli, uamsho.

³ Niliangalia wakati mmoja kwenye ufuko wa bahari, ambapo upepo ulikuwa ukivuma, nao ulikuwa tu ukitingisha. Mbona, haikuwa ni ufuko wa bahari, ilikuwa ni—ilikuwa huko Ziwa Michigan. Nilikuwa nimesimama pale nikiangalia mawimbi wakati yakiingia, na—na, loo, bahari hiyo ilikuwa ikiruka, ama maji yalikuwa yakiruka, na—na mashua zikirukaruka. Nami nikawazia, “Ni kitu gani hicho kinachoendelea?” Nikawazia, “Mbona, ziwa hili linakuwa na uamsho.” Jambo ndilo hilo. Linarukaruka na kutikisika, kwa nini? Kuna upepo wenye nguvu ukienda kasi unaoshuka juu yake. Nikawazia, “Vema, unajua nini? Hakuna tone moja zaidi la maji ndani yake sasa zaidi ya jinsi lilivyokuwa wakati lilipokuwa shwari kabisa. Hamna maji

zaidi ndani yake; limetibuliwa tu kabisa. Vema, sasa, limetibuka kwa nini?” Unajua kutibuka kwa maji kunafanya nini? Huondoa takataka zote toka kwake, zikapelekwa ufukoni.

⁴ Hilo ndilo tunalohitaji, kuondolewa kwa kutokuamini, kufagiliwa ufukoni. Kuruhusu Neno la Mungu lipate utangulizi. Hilo ndilo tunalohitaji, uamsho, na kuondolewa kutokuamini kote, na wadudu wote na ushirikina, na kadhalika. Tutoke nje na tuone ya kwamba Mungu angali ni Mungu. Hiyo ndiyo sababu tunakuwa na miamsho.

⁵ Bwana na atusaide tunapochagua somo hili na kulisoma kwa usiku wa leo. Bwana na abariki kusomwa kwa Neno Lake, linalopatikana katika Mathayo Mtakatifu, mlango wa—wa 12, kifungu cha 38 na hadi kifungu cha 42.

⁶ Na somo langu usiku wa leo ni: *Uwepo Wa Mungu Usiotambuliwa*. Jana usiku tulikuwa tukizungumza kuhusu Yesu kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na tukaona ya kwamba alikuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa Uwepo Wake, kama ni yeye yule, hautambuliwi. Hebu na tusome.

Hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.

Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara; wala hakitapewa ishara; ila ishara ya nabii Yona.

Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.

Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.

Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki; naye atawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani, na hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

⁷ Uwepo Usiotambuliwa! Watu hawa wangukuwa wakifikiria nini? Mungu daima, imekuwa hivyo kila wakati anapokuja. Wakati Yesu alipokuwa hapa mara ya kwanza, Yeye alisema, “Ninyi—ninyi mnayapaka chokaa na kuzipamba kuta na makaburi ya manabii, nanyi ndinyi mliowaweka mle.” Unaona, jambo fulani hutukia, nalo linapita. “Na Mungu analificha kutoka kwa macho ya wenye hekima na akili, na kuwafunulia watoto wachanga watakaojifunza.” Yesu alimshukuru Baba kwa

kufanya jambo kama hilo. Mnaona? Linawapita tu watu wala hawajui.

⁸ Kwa mfano, ninyi Wakatoliki hapa usiku wa leo, mnakumbuka miaka michache iliyopita, Joan wa Arc, huko Ufaransa, maskini msichana yule ambaye kweli alikuwa... Yeye aliyaongoza mapinduzi huko Ufaransa, bali yeye kweli alikuwa ni—ni mtumishi wa Kristo. Kanisa lenu lilimfanyaje? Lilimchoma kwenye nguzo, kama mchawi, kwa kuwa aliona maono na alikuwa wa kiroho. Kanisa Katoliki lilimchoma moto, kama mchawi, kwenye nguzo, kwa kuwa alikuwa ni wa kiroho na aliona maono. Miaka michache baadaye, waliona kwamba mwanamke huyo alikuwa ni mtakatifu. Kwa hiyo bila shaka mlifanya kitubio kikubwa, mliichimbua miili ya hao makasisi waliomhukumu na kumchoma moto, kisha mkaitupa mtoni. Hakika, hilo, mlifanya kitubio kikubwa kwa ajili ya jambo hilo, kwa kuichimbua miili ya makasisi hawa.

⁹ Sasa, katika siku za manabii, ni jambo gani lililotukia? Walifanya jambo lile lile. Hawakuwatambua mpaka walipokwisha kuja, wakamaliza huduma yao, wakawachukua hao Wateule, halafu wakiisha kuondoka wakatambua ya kwamba kulikuwako na nabii miongoni mwao.

¹⁰ Yesu, Yeye alikuja duniani. Ndani Yake alikirimiwa kuwa na Baba, Mungu. “Mimi na Baba Yangu ni mmoja. Baba Yangu anaishi ndani Yangu. Si Mimi nizifanyaye hizo kazi, bali Baba Yangu. Na kama sizitendi kazi za Baba Yangu, msiniamini.” Sasa, kama mkiangalia wakati alipokuja, kadiri ya mmoja—mmoja katika tisini ya watu wa ulimwengu alijua ya kwamba Yeye hata alikuwa duniani wakati huo, na hata hivyo ni Mwokozi wa ulimwengu. Halafu basi hawakutambua kwamba Yeye alikuwa ni nani, hata kanisa ama yeyote yule, ilikuwa ni vigumu, mpaka walipokuwa wamemsulibisha, wakamzika, na akafufuka katika siku ya tatu, kabla kamwe hawajatambua kwamba Yeye alikuwa ni Nani.

¹¹ Linakuja na kuondoka, na watu hawalitambui mpaka limepita, na, wao, kwa kuwa kamwe haliendani na theolojia yao, haliendani na wakati wa siku hiyo. Mnaona, jambo ni kwamba, wao daima wanaishi katika mng’ao mkali wa wakati mwingine, sikuzote.

¹² Sababu ya wao kutokumkubali Yesu, kwa sababu walikuwa wakiishi katika mng’ao wa Torati. Na wakati Yesu alipokuja, haikuwa ni kinyume na Torati, bali alikuja kuitimiza Torati, vema, hawakuweza kumkubali kwa sababu Ujumbe Wake haukuwa jinsi hasa walivyokuwa wameupangilia kwenye kanuni zao za imani, na ziliitwa basi mapokeo. Na Yeye hakuja kulingana na mapokeo yao. Hakuweka mapokeo yao. Na kwa kweli aliyavuruga, na kuyararulia mbali, na—na kufanya mambo yaliyokuwa ni kinyume nayo, hivi kwamba walidhani alikuwa

anayavunjilia mbali makanisa. Wala wasingeweza kumpokea kwa sababu ya Ujumbe Wake. Nasi sote tunajua siku hizi ya kwamba Yeye alikuja kulingana kabisa na unabii wa Mungu, bali hawakujua hilo wakati huo.

¹³ Nalo laweza kutukia tena, wala tusingeweza kujua. Ninawazia kama kweli angetokea usiku wa leo, ingekuwa ni kinyume sana na vile tumeyapanga kwenye chati zetu, na katika shule zetu na kadhalika. Ni wachache sana wangetambua kilichokuwa kikiendelea. Yeye alisema ingekuwa hivyo, jinsi alivyokuja.

¹⁴ Sasa, Yesu akiwa pale ametambulishwa kwa udhahiri sana Kimaandiko na Maandiko, nao Waandishi na Mafarisayo wa siku hizo hawakuweza kumtambua. Ni kwa nini hawakumtambua, kwa nini hawakufanya hivyo? Kwa sababu walikuwa wameliwazia vinginevyo. Hapo ndipo Yesu alipowaambia, “Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani yake mnadhani mna Uzima wa Milele, nayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi.” Unaona? Sasa Yeye alikuja kulingana kabisa na Maandiko. Lakini wao walikuwa wameliwazia kwamba labda kama angekuja, Masihi huyo labda angefanya yale Musa aliyofanya, ama yale Nuhu aliyofanya, kuwajengea safina ama kitu, kingine. Lakini, sababu ya Yeye kuja jinsi alivyokuja, wao hawakuwa wameliwazia; katika Maandiko pamoja na mapokeo yao, hawakuyafundisha; kwa hiyo watu walikuwa wamechanganyikiwa sana hawakujua kile kilichokuwa kikiendelea.

¹⁵ Sijui kama hilo lingeweza kutukia leo? Sijui kama lingeweza kuwa ni tofauti na vile mapokeo yetu yametufundisha? Nalo lingeweza kuja, na kitu fulani kingepitia hapa na tusingeweza hata kujua mpaka kimekwisha kupita tayari, na ndipo jambo limekwisha. Hivyo ndivyo karibu jinsi litakuja.

¹⁶ Je! unajua, wakati Yohana mbatizaji alipojitokeza jukwaani, hilo lilikuwa limebashiriwa kote kote kutoka Kitabu cha Isaya, mamia ya miaka? Karibu miaka mia nane, Isaya alitabiri, nafikiri, kabla ya kuja kwa Kristo. Hivi mlijua Yohana alikuja vile vile hasa Isaya alivyosema angekuja, alikuja vile vile hasa Malaki alivyosema angekuja, na hata mitume hawakutambua hilo? Siku moja, katika Mathayo 11, Yohana alikuwa gerezani; nao mitume, baadhi ya mitume wake walienda kule kumwuliza Yesu kama Yeye alikuwa Ndiye, ama—ama wamtazamie mwingine.

¹⁷ Sasa angalieni, Yesu hakuwapa kitabu cha jinsi ya kujiadibisha mwenyewe, jinsi ya kujiadibisha gerezani, ama jinsi ya kuenenda kitabia. Alisema, “Kaeni hapa mwone kile kinachotendeka, kisha mwende mkamweleze Yohana mambo mliyoyaona yakitendeka.” Huo ulikuwa ndio ushahidi ya kwamba ninii . . . Yeye alikuwa ni hilo Neno.

18 Na sasa kumbukeni, Neno daima humjia nabii. Sisi sote tunajua hilo. Mungu hatendi neno bila ya kuwaonyesha manabii Wake. Hiyo ndiyo sababu Kitabu cha Ufunuo wa Yesu Kristo ndio utimilifu kamili wa Kristo papa hapa mbele zetu, hicho Kitabu. Sasa itambidi kumtuma mmoja, mtu fulani akakithibitishe hicho Kitabu, akakifunue, akaifungue Mihuri, na kadhalika. Lakini kuhusu ufunuo wowote wa zaidi wa Kristo, tayari umetambulishwa moja kwa moja Humu. Yeye Ndiye utimilifu wa Hili, wa Ufunuo. Sasa angalieni, kamwe halishindwi, bali Neno humjia nabii.

19 Hebu mwangalie Yohana akisimama majini, akibashiri, yule nabii, ya kwamba Masihi alikuwa papo hapo miongoni mwao. Alisema, “Yupo Mtu anayesimama miongoni mwenu sasa, msiyemjua; Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto.” Sasa kumbukeni, Yeye alikuwa amesimama papo hapo miongoni mwao, Biblia ilisema hivyo, wala hawakumtambua. Siku moja wakati Yesu alipokuja akitembea kule, Yohana alimtambua, naye akasema, “Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu.” Sasa angalia, kabla hajatambuliwa na mtu yeyote, Yeye alimjia nabii. Yeye alikuwa ni Neno. Yohana alikuwa ni nabii.

20 Ninakumbuka maskini mwalimu wangu wa Kibaptisti aliniambia, kasema, “Unajua ni jambo gani lililotukia?” Kasema, “Yesu alimbatiza Yohana.”

Nikasema, “Sidhani alimbatiza.”

21 Akasema, “Hakika, Yohana hakubatzwa kamwe; alikuja akihubiri, akibatiza, hakuna mtu aliyestahili kumbatiza. Yesu alimbatiza.”

Nikasema, “Sijui.”

22 Basi siku moja nikiwa katika kusoma, Roho Mtakatifu alilifunua namna hii, mnaona. Tazameni, Yeye alienda akaingia majini; akasema, “Kwa nini wanijia mimi? Ninapaswa kubatzwa na Wewe.” Yesu akasema, “Kubali iwe hivyo,” angalia, “lakini inatupasa (inatubidi) kuitimiza haki yote.” Yohana, akiwa ni nabii, akijua Neno! Dhabihu aliyekuwa ni Yeye, haina budi kusafishwa kabla haijatolewa; ndipo alibatizwa, Yohana alimbatiza, kwa sababu, “Inatupasa tuitimize haki yote.” Neno lilimjia nabii, majini.

23 Na ndipo wakati alipobatzwa, bado watu... Ndipo Roho Mtakatifu akashuka, si kila mtu alimwona. Yohana alimwona.

24 Malaika wa Bwana angeweza kuwa hapa usiku wa leo, na labda mtu mmoja amwone, wala si mtu mwingine.

25 Ile Nuru, ile Nyota iliyopitia kwenye kila chumba cha uchunguzi, ambapo wa—wale mamajusi walifuata; hakuna chumba cha uchunguzi kinachojua lolote kuihusu, hakuna mtu mwingine yeyote aliyeiiona, hata kidogo, ila hao mamajusi, kwa

maana ilikuwa ni kwa ajili yao waione. Waliiona. Ilikuwa ni halisi kwao.

²⁶ Wakati ile Nuru, ile Nguzo ya Moto, ilipompiga na kumwangusha Paulo, akienda zake Dameski, yeye alitambua ya kwamba alikuwa katika Uwepo wa Mungu. Sasa, Mwebrania huyo kamwe asingeiita roho nyingine yoyote, “Bwana,” vile vile yeye alijua Hiyo ilikuwa ni Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza watu wake kutoka nyikani. Alisema, “Bwana, U Nani Wewe?”

“Sauli, Sauli, mbona waniudhi?” Akasema, “Mimi ni Yesu.”

²⁷ Yesu akasema, “Nilitoka kwa Mungu, nami narudi kwa Mungu.” Yeye alikuwa ule Moto uliokuwa kwenye Kijiti kilichowaka moto, uliomwongoza Musa nyikani, Naye alirudi tena kwenye Huo.

²⁸ Na sasa huyu hapa, njiani akienda zake Dameski, alikuwa amepigwa akaanguka. Na watu wote waliokuwa pamoja naye, hawakuiona kabisa hiyo Nguzo ya Moto. Nayo i—ilikuwa ni halisi sa—sana kwa Paulo mpaka ikampofusha, naye ilibidi aongozwe apelekwe kwenye mtaa ulioitwa Mnyofu, huko Dameski. Alikuwa kipofo.

²⁹ Anania, nabii kule chini, aliona katika ono, alienda akamwekea mikono naye akampokea Roho Mtakatifu, nayo magamba yakaanguka kutoka machoni mwake na angeweza kuona tena. Ilikuwa ni halisi sana kwake hata ikayapofusha macho yake, na hata hivyo hakuna mtu kati ya hao wengine aliyetambua ilikuwa pale, angeweza kuiona.

³⁰ Kadhalika—hali kadhalika ndivyo ilivyo usiku wa leo! Kuna mtu anayeketi papo hapo anayeweza kumleta Mungu jukwaani, wakati huyo mwingine hatajua lolote kulihusu. Kumtambua Mungu!

³¹ Na Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, na alikuwa amefanya kabisa ishara ambayo Biblia ilisema angeifanya, lakini hawakulitambua hilo kwa sababu halikuwa ni kulingana na mapokeo yao. Kwa wakati huo, Yeye hakuwa aje akafanye yale Musa aliyofanya. Alikuwa aje na azaliwe na bikira. Naye, na kulingana na Kumbukumbu la Torati 18:15, Yeye alikuwa awe ni nabii. Na hakika Yeye alifanya kazi hizo na ishara.

³² Wayahudi daima walitafuta ishara. Walifundishwa kamwe wasitegemee hotuba za elimu; Wayahudi walijua vema zaidi kuliko hivyo. Wayunani walifundisha jambo hilo. Lakini si hotuba za elimu, bali juu ya ishara. “Utuonyeshe ishara.” Hawa watu, mmoja alisema, “Rabi, ama Mwalimu, utuonyeshe ishara.” Walitaka kujua. Naye tayari alikuwa amewaonyesha ishara, nao walitaka ishara ya aina nyingine, bali yeye aliweza tu kufanya ishara ya wakati huo.

³³ Vilevile ndivyo afanyavyo siku hizi, huku kumwagwa kwa Roho Mtakatifu ni ishara ya kuonekana Kwake hata katika wakati huu, kama Yeye alivyoahidi.

³⁴ Wao wanataka ishara, Naye alikuwa amewapa ishara ya Kimaandiko, bali wao walitaka ishara ya tofauti.

³⁵ Hapo ndipo ambapo watu wengi sana siku hizi watachanganyikiwa. Mwajua, Unyakuo huenda ukatukia, na wazieni tu huzuni yake! Hebu nirejee nyuma ambapo Yesu, ama...

³⁶ Yohana aliwatuma wanafunzi wake kwenda kumwona Yesu, kama Yeye alikuwa ni Masihi ama siye. Saa hiyo, alifanya mambo mengi. Aliporudi, hao wanafunzi, kumwambia Yohana yale waliyokuwa wameona, Yesu akawaambia hao waliokuwa wameketi pale, kasema, “Mlitoka kwenda kuona nini nyikani? Mlitoka kwenda kuona nini wakati Yohana alipokuwa akihubiri? Je! mlikwenda na kumwona mtu aliyevikwa mavazi meupe, na kadhalika, ama—ama mavazi mororo?” Kasema, “Hao ndio ninii... wako katika nyumba za wafalme. Wanazika wafu, na kubusu watoto wachanga, na kuwaoza vijana, na kadhalika, namna hiyo. Hawajui kuutumia upanga wenye mikono miwili.”

³⁷ Kasema, “Mlitoka kwenda kuona nini basi, unyasi unaotikiswa na upepo wowote, mtu fulani, kundi fulani litampa fedha nyingi zaidi kidogo naye atahamia kwa *hili* badala ya kuufuata wito wa Bwana? Si Yohana!” Mtu fulani angeweza kumgeuza huku, aseme, “Tutakupa zaidi kama utakana *Hili* na kulichukua *hili*?” Si Yohana!” Akasema, “Mlitoka kwenda kuona nini basi, nabii?” Akasema, “Nawaambia, ‘zaidi ya nabii.’ Na kama mnaweza kulipokea, huyu ndiye ambaye nabii alisema, ‘Tazama, ninampeleka mjumbe Wangu mbele za uso Wangu, ambaye ataitengeneza njia.’” Na hiyo ilikuwa ni Malaki 3, ambapo alilisema.

³⁸ Siku moja wanafunzi walimwuliza, wakasema, “Kwa nini Waandishi walisema kwamba Eliya hana budi kuja kwanza?” Yesu akasema, “Amekwisha kuja tayari wala hamkujua,” nao wakafahamu ya kwamba ilikuwa ni Yohana Mbatizaji. Wale mitume walioteuliwa wangali hawakuweza kuona yeye alikuwa ni nani. Huyu alikuwa ni Eliya.

³⁹ Sasa angalieni. Mnajua, Ku—Kuja kwa Bwana kutakuwa ni kuja kwa siri. Yeye alisema, “Kutakuwako na wawili kitandani, nami nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja,” hiyo ni sehemu i—iliyo usiku. “Wawili kondeni, nitamchukua mmoja na kumwacha mmoja.”

⁴⁰ Mnajua, kuna watu wengi sana wanaopotea kila siku, kutoka usoni pa nchi, hata hakuna mtu anayeweza kujua waliko. Moja ya siku hizi huenda ikawa watu huenda wakasema, “Vema, unamaanisha ile dhiki, kitu hicho kimetupata sasa? Nilidhani ilibidi Kanisa liondoke kabla ya ile dhiki.” Hawatambui na

kufahamu ya kwamba Unyakuo ungeweza kutukia wasijue kitu kuuhusu; ni kule kuondoka kisiri kwa Kanisa.

⁴¹ Na, wazieni, watu wataendelea kuhubiri moja kwa moja, wakisema wanaamini wanaokoka, na kuongezea kwa kanisa, na kujenga makanisa, na kuendelea kama tu walivyofanya katika siku za Nuhu, na kadhalika, wala wasijue; na Unyakuo umekwisha kupita, “umekwisha kutukia nanyi hamkujua.” Kuna mamia ya watu wanaopotea kutoka duniani na watu hawajui kitu kuhusu walikoenda, hawawezi kujua waliko; mtu fulani alikuwa akienda mahali fulani, hawasikii habari zao tena. Basi huo unaweza kuwa ni Unyakuo.

⁴² Nawaambieni, enyi marafiki, kwamba tu sisi ni wafuasi wa kanisa, ama kitu kama hicho, hilo halimaanishi mengi sana kwetu. Afadhali ujifunge silaha hiyo. Afadhali ulichukue Neno hilo lote la Mungu na kulishikilia, na uachane na huku kutenda kama Hollywood hapa. Imeingia moja kwa moja kanisani, na ni fedheha. Lakini Hollywood hung’aa, inafanya tu nuru angavu, nalo kanisa siku hizi linajaribu kujilinganisha na Hollywood. Kristo hayuko Hollywood. Kristo yumo ndani ya mtu binafsi. Hollywood humeka... ama Hollywood hutoa mng’aro mkali, wakati Injili inameka kwa unyenyekevu. Mungu hayuko kwenye sehemu hizi kuu nzuri zenye madoido na upuuzi huu wote tunaouona. Yeye huingia katika unyenyekevu, katika hali ya upole na unyenyekevu, anapita moja kwa moja.

⁴³ Na kama unalifahamu Neno, utalionga. Yeye aliye na jicho, kusikia, “na alisikie lile ambalo Roho ayaambia makanisa,” mnaona sasa, sasa leo, ambalo lilithibitisha.

⁴⁴ Yeye alijitambulisha kikamilifu kwa waaminio siku hiyo, hao waliokuwa wakilitazamia. Hebu mwangalie Petro na Andrea. Mwangalie Nathanaeli, hakuna swali niani mwake. Mwangalie yule mwanamke kisimani, hapakuwapo na swali katika jambo hilo.

⁴⁵ Lakini hawa Mafarisayo, siku chache kabla ya mahali lilipo somo letu usiku wa leo, walimwona akifanya jambo hilo, ndipo wakamwita “Beelzebuli, ibilisi.” Kazi zilikuwa zimefanywa. Ilibidi kulielezea kusanyiko lao, kwa hiyo jambo pekee wangiaweza kufanya lilikuwa ni kuliita “pepo mchafu.” Beelzebuli alikuwa ni ibilisi, kama vile mpiga ramli ama kitu fulani. Na mtu yeyote anajua ya kwamba kupiga ramli ni kwa ibilisi. Nao walikuwa wakilinganisha, ambapo Yeye alikuwa ni Neno lililoiujua siri ya moyo na ni—na linathibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Nabii yule ambaye alikuwa ainuliwe kwetu katika siku hizi, Nabii-Mkombozi; na alipofanya hivyo, kanisa katika siku hiyo lilimtangaza kuwa ni “Beelzebuli.”

⁴⁶ Mnaona kile walichokuwa? Yeye alisema, “Ninyi ni vipofu, mkiwaongoza vipofu.” Hawataingia, wala hawawaruhusu wale walio chini yao waingie.

⁴⁷ Kile tunachotaka kufanya siku hizi ni kupata ile Kweli. Hatuna budi kuijua Kweli. Je! Yeye ni yeye yule? Je! Yeye yupo hapa kuyatimiza yale aliyoahidi kutimiza? Yachunguzeni Maandiko na mwone kile anachopaswa kufanya siku hizi.

⁴⁸ Hiyo ndiyo sababu ambayo John Wesley...ama Martin Luther asingeweza kuendelea na ujumbe wa Wesley; wao waliuundia dhehebu, huo ndio umbali lingaliweza kwenda. Ndipo akaja Luther, kutoka kwenye kanisa Katoliki, naye wao... Yeye alikuwa mwendawazimu, kwao; bali alikuwa ana ujumbe wa kuhesabiwa haki maana ulikuwa ni Neno la Mungu, ahadi. Ndipo wao, baada ya kifo chake, waliliunda dhehebu la Luther. Basi nini kilitukia, lote likajikunyata tena.

⁴⁹ Na kulingana na Maandiko hapana budi painuke wakati mwingine wa kanisa, na, wakati lilipoinuka, ule Wakati wa Kanisa la Filadelfia ulikuja, John Wesley. Na jambo lililotukia, liliendelea kuja magharibi wakati wote. Na wakati lilipotukia, kulikuwako na wakati wa kanisa, ndipo John Wesley akainuka, bali Luther asingeweza kulipokea kwa sababu tayari walikuwa wamejiundia dhehebu la kuhesabiwa haki. Asingeweza kuupokea utakaso.

⁵⁰ Ndipo wakati Wawesley walipojiundia dhehebu jinsi walivyojiundia, na matawi madogo yakatokea, ambayo yalitokea, ndipo ukaja ujumbe wa Kipentekoste wa kurudishwa kwa karama; hakuna moja la hayo lingaliweza kusogea, walikuwa tayari wameunda madhehebu.

⁵¹ Sasa sehemu yake ya kuhuzunisha ni kwamba, Wapentekoste hali kadhalika walijiundia madhehebu.

⁵² Hebu angalieni siku tunayoishi, kile kilichoahidiwa kwa ajili ya siku hii. Tuko wapi? Tumepanda juu. Nguzo ya Moto inasogea, nao wana wa Israeli wakasogea pamoja na Nguzo ya Moto vinginevyo walirudi Misri. Hatuna budi kusogea pamoja na Neno.

⁵³ Na leo tunakuwa wavivu sana, kanisa linakuwa la kilimwengu sana na lisilojali sana, na kwa hiyo nia zao zimepotoshwa sana na televisheni, na *Tunampenda Susi* na baadhi ya mambo haya machafu, na kukaa nyumbani. Hilo linaonyesha mahali mioyo ya watu ilipo. Na mtu unaweza kuwaambia mambo haya ni mabaya, nao wanafikiri wewe ni mwendawazimu. Ni kitu gani? "Wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu." Mnaona?

⁵⁴ Loo, raha kubwa sana niijuayo, ni kuwa kuomba mpaka niweze kutambua ya kwamba niko kwenye Uwepo wa Mungu, na kutambua hilo. Nafikiri hilo linapaswa kuwa ndiyo furaha ya Kanisa, ni Uwepo wa Roho Mtakatifu; kumwona Mungu aliyeitoa ahadi amesimama miongoni mwetu, kuuhihi Uwepo Wake na kuliona Neno Lake, na kuliona likithibitishwa.

Linapswa kutoa imani, kuwafanya viwete kutembea, vipofu kuona, viziwi kusikia, bubu kusema.

⁵⁵ Nilisimama huko Afrika Kusini, ambako nilikuwa na watu mia mbili elfu kwenye uwanja wa mbio huko Durban, na walipoona wakati mmoja hilo likitukia jinsi hiyo, baada ya kuwaelezea hilo, kwa njia ya upole tu; nao wakaona jambo moja likitukia, la hayo kufunuliwa, na watu elfu ishirini na tano waliponywa papo hapo mara moja. Waliokota malori saba, malori hayo ni marefu kama kutoka *hapa*, yenye magurudumu sita na kumi na manane namna hiyo, nayo yamejazwa kabisa na magongo na kadhalika. Makafiri, ambao hata hawakujua mkono wao wa kuume na wa kushoto ulikuwa ni upi.

⁵⁶ Ndipo kesho yake, Bw. Sidney Smith, meya wa Durban, alinipigia simu na akasema, “Nenda kwenye dirisha lako, linaloelekea Bahari ya Hindi, utaona kitu ambacho hujapata kuona.” Na hicho kilikuwa ni polisi wakisindikiza hayo malori saba makubwa yaliyojaa, huku mamia ya watu wakitembea kwa miguu nyuma yake, ambao siku moja kabla walikuwa kwenye machela na vitanda na vibebaji walivyokuwa navyo, wakiimba, “Amini tu, mambo yote yawezekana.” Juma moja hapo kabla, kule, walikuwa wakipigana vita, vita vya kikabila. Nao hawa hapo walikuwa wanatembea, wameshikana mikono, mkono kwa mkono.

⁵⁷ Kwa nini? Walitambua Mungu wa Mbinguni alikuwa ameonekana mbele zao katika jinsi ya Neno Lake. Na sisi Wamarekani wasomi tunaketi kitako. Watasimama kwenye ile Siku ya Hukumu na kukihukumu kizazi hiki, kwa yale tumeona.

⁵⁸ Inanikumbusha juu ya mwanamke mmoja huko Louisville, Kentucky, sio muda mrefu uliopita, alikuwa na mtoto mchanga, akitembea kwenye duka kubwa la mali rahisi. Naye alikuwa akifanya mambo madogo, akijaribu kumfanya aone, naye maskini mtoto huyo mchanga akaendelea kukaza macho tu mbele. Basi hatimaye akachukua kengele ndogo, kitu chochote kinachopaswa kuvutia macho ya maskini jamaa mchanga wa kimo hicho. Basi akaitingisha kengele hiyo, naye maskini jamaa huyo mdogo alikaza tu macho moja kwa moja mbele. Ndipo akaanza kupiga mayowe, na akaanguka, ndipo baadhi ya watu wakaja kumsaidia. Akasema, “Loo, la, haiwezekani! Haiwezekani!”

Wakasema, “Kuna nini?”

Akasema, “Daktari alisema mtoto amepata nafuu.”

Wakasema, “Kwani mtoto ana shida gani, mama?”

⁵⁹ Kasema, “Vema, alipatwa na degedege yapata miezi sita iliyopita, kwamba anaketi tu na kukodoa macho. Haidhuru ni kitu gani, kinachopaswa kuvutia macho ya mtoto huyo mchanga, hakitavutia macho yake, naye anaketi tu na kukodoa macho. Daktari aliniambia alidhani alikuwa amepata nafuu.

Nami nikamleta huku, kuchukua vikorokoro vidogo ambavyo vinapaswa kuvutia macho ya mtoto huyo, wala haviyavutii. Angali anaketi na kukodoa macho.”

⁶⁰ Hivyo ndivyo kanisa linavyopata kuwa! Mungu ametingisha kila ahadi katika Biblia, mbele zao. Tungali tunaketi tu na kukodoa macho, tukiangalia. “Ati nini? Nionyeshe ishara, utanionyesha?” Na inaendelea wakati wote, kote karibu na sisi. Kuuleta Uwepo wa Mungu, linapaswa kutuangazia. Wakati Mungu alipotoa ahadi, Yeye anasimama na ahadi hiyo. Naam, bwana.

⁶¹ Baada ya Yesu kuithibitisha ishara Yake ya Masihi, ya kwamba Yeye alikuwa ndiye huyo Masihi, hata hivyo mbele ya hayo yote, “Tuonyeshe ishara.” Mnaona, hawakutambua, walikuwa tu wamekaza macho yao mbele. Haikuwa ndani yao kuamini.

⁶² “Wewe,” kama maskini mama yangu wa kusini alivyo zoea kusema, “huwezi kupata damu kutoka kwenye tanipu, maana hamna yoyote mle.”

⁶³ Wangali hawakumtambua, walikuwa wamepofushwa sana na kanuni zao za imani na—na—na kadhalika, walizokuwa nazo siku hiyo. Hawakuyajua Maandiko ya ahadi, kwa kuwa kanuni za imani zilikuwa zimeifunika. Kanuni zao za imani na mapokeo ya siku ile zilikuwa zimeifunika ahadi ya Maandiko. Laiti wangelikuwa wamefundishwa kulingana na Maandiko, ya kwamba hiyo ilipaswa kuwa ndiyo ishara iliyomfuata Masihi!

⁶⁴ Ni wangapi wanaamini ya kwamba alikuja katika ishara Yake sahihi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakika, alikuja, alikuja kulingana na ahadi. Bali walikuwa wamefundishwa kanuni ya imani, “Tunaamini katika *hili*, na tunaamini katika *lile*. Wote wanamwamini Mungu. Wote . . .”

⁶⁵ Leo hii, sisi Wamarekani, hasa, tunafikiri ya kwamba tutawiwa radhi kwa kuwa tunajenga makanisa makubwa, na tuna wachungaji wazuri na kadhalika. Kumbukeni, kama hivyo ndivyo ilivyokuwa, Mungu hana haki kama akituchukua jinsi hiyo; kwa kuwa, Kaini na Habili, wale waabudu wawili wa kwanza nje ya Edeni, walimjengea Bwana madhabahu, wote wawili walitoa dhabihu, wote wawili walitoa matoleo, wote wawili waliomba, bali mmoja alikuwa mwenye haki na huyo mwingine alikuwa mwovu. Angalieni, hatuna budi kuwa na Kweli, nayo Kweli ni Neno la Mungu, daima. Sasa ni vivyo hivyo leo, watu wanakuwa wamepofushwa sana. Wanasema . . .

Ninasema, “Je! wewe—wewe ni Mkristo?”

⁶⁶ “Loo, mimi ni mfuasi wa kitu fulani-fulani.” Mnaona, hilo halina uhusiano wowote nalo. Sina neno dhidi ya hilo, bali hilo silo ninalojaribu kuwaambia. Kuwa mfuasi wa kanisa lolote unalotaka. Chapa yako haileti tofauti yoyote.

⁶⁷ Nilikuwa nikimwambia mchungaji asubuhi ya leo. Huko Colorado nilikuwa nikiwakusanya ng'ombe kwa farasi, na kadhalika. Nami nilikuwa nikiketi pale, mguu wangu kuingama tandiko la farasi, namna *hiyo*. Na Shirika la Hereford la Mto Msumbufu huwalisha kwenye Bonde la Mto Msumbufu. Ndipo ukikwea juu ya hilo bonde, una mkondo wa mashariki na wa magharibi. Ng'ombe wote kutoka *hapa* kwenda juu, kwenye Shirika hilo, hulishwa kwenye mkondo wa magharibi; na—na kundi nililokuwa pamoja nalo, walilisha kwenye mkondo wa mashariki. Halafu walikuwa na kizuizi cha ua pale kuwazuia hao ng'ombe wasiingie kwenye mali ya binafsi, na kukwea milimani katika msimu wa kiangazi.

⁶⁸ Nasi tungewakusanya hao ng'ombe, aina nne ama tano mbalimbali, aina nane ama kumi mbalimbali, huko mtoni, tungewakusanya hao ng'ombe katika msimu wa kuchipua, tuwapeleke huko juu. Nami nilikuwa nikiketi pale, mguu wangu kuingama ncha ya tandiko la farasi, baada ya sisi kuwakusanya ng'ombe wote, wote walikuwa wametiwa chapa na kila kitu, wakipelekwa malishoni.

⁶⁹ Naye mpanda farasi alisimama pale. Alikuwa akiwahesabu wakati wakipita. Nami niliona kulikuwako na kila aina za chapa. Bw. Grimes alikuwa na—na—na Tepe Almasi, na papo hapo juu yetu tu kulikuwako na Wayo Batamzinga, sisi tulikuwa na Migutatu Kizee, na kulikuwako na chapa mbalimbali zilizopitia pale. Ila yule—yule mpanda farasi hakujali chapa hizo. Aliangalia kishikizo cha damu sikioni. Hakuna kitu kingaliweza kuingia kwenye malisho hayo, kuhifadhi mashirika ya uzalishaji, kudumisha ng'ombe wao na ukoo bora, hakuna kitu kingelienda kule ila ukoo bora wa Hereford. Ilibidi wabandikwe kishikizo sikioni, kwa alama ya damu.

⁷⁰ Hivyo ndivyo itakavyokuwa kwenye ile Hukumu. Yeye hataniuliza kama nilikuwa M—Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri. Chapa niliyo nayo haitamaanisha kitu Kwake. Hakuna chochote ila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, kwa Damu ya Yesu Kristo, huyo ndiye atakayeingia. Hakuna kitu kingine pungufu ya hicho kitakachoingia ndani. Sasa tunataka kukumbuka, kukumbuka jambo hilo.

⁷¹ Sasa, wakati Yeye hatambuliwi, nguvu Zake dai-...daima hazifunuliwi, wakati Yeye hatambuliwi. Haidhuru ni kiasi gani cha Mungu kimesimama hapo, huna budi kuamini hilo. Hivyo tu.

⁷² Ni kama yule mwanamke aliyekuwa na kutokwa na damu. Hao watu wote wakipita pale, na hao wote wakisimama, wakisema, “Yule pale Rabi anaenda. Yule pale Jamaa anayedai kwamba ni Nabii. Huyu ni yule mlokole,” na mambo yote kama hayo.

⁷³ Lakini ni jambo gani lililotukia? Maskini mwanamke huyu alikuwa akitokwa na damu, naye alikuwa amesikia habari Zake. Na aliposhuka kuja pale, haidhuru mtu yeyote alisema nini, yeye alitambua kwamba alikuwa ni Nani. Na akasema, “Ikiwa tu ninaweza kugusa vazi Lake!” Mnaona?

⁷⁴ Na wakati hiyo imani halisi, katika Mungu, ilipofanyika jambo halisi kwake, ilifungulia kitu gani? Ilizifungulia nguvu Zake za kumponya. Ilingusa kwa njia fulani hivi kwamba, Yeye aligeuka na kumwambia shida yake ilikuwa ni nini, kasema, “Imani yako imekuokoa.” Ni kitu gani kilicholifanya? Imani!

⁷⁵ Wengine waliosimama pale huenda walikuwa ni wagonjwa zaidi kuliko yeye, lakini, unaona, yeye aliutambua Uwepo Wake. Alijua hiyo ilikuwa ndiyo nafasi yake.

⁷⁶ Laiti tungaliweza tu kufanya hivyo usiku wa leo, enyi watu! Laiti tungaliweza kutambua ya kwamba Yeye anatutokea katika mikutano hii, kwa kusudi moja, hilo ni, kuachilia shauku tulizo nazo ndani Yake, kwetu. Lakini hatuna budi kuutambua Uwepo Wake. Na sasa jinsi unavyoutambua Uwepo Wake, ni wakati Neno lililoahidiwa kwa wakati *huu* linapodhihirishwa, sio Neno lililoahidiwa la Wakati wa Musa, ama wowote wa nyakati zingine, ahadi ya Neno la wakati *huu*!

⁷⁷ Sasa tunaona Yeye aliendelea moja kwa moja. Na Yairo, maskini jamaa mdogo huko juu akiwa na binti aliyekufa, yeye binti, yeye baba aliamini yale aliyosema yalikuwa ni Kweli. Sasa kumbukeni, yeye alikuwa ni kuhani, naye alikatazwa, maana ilikuwa imetangazwa vikali, “mtu yeyote aliyeshirikiana na Yeye angefukuzwa kutoka kwenye sinagogi.” Vema, kama alifukuzwa ama kama hakufukuzwa, yeye aliridhika ya kwamba Mungu alikuwa yumo ndani ya Kristo, na Huyo alikuwa ni Neno. Nalo lilifanya nini? Lilimfungulia nguvu za ufufuo zilizokuwa ndani Yake; amina, zikamfufua msichana aliyekuwa amekufa, na kulazwa huko, kwa sababu yeye alitambua ya kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo, na Uwepo Wake ulikuwa ndani ya nyumba yake.

⁷⁸ Lakini katika mji alimolelewa, nguvu zizo hizo zilikuwa ndani Yake, kwenye mji alimolelewa, bali kamwe wao hawakumtambua. Uwepo Wake, kwao, haukumaanisha kitu; labda ni mlokole fulani. “Mambo haya yako wapi? Wananiambia ya kwamba Wewe unafanya *hili na lile*. Hebu nikuone ukiyafanya hapa.”

⁷⁹ Hivi hamjasikia hayo? “Kama kuna...Ninyi kundi la wapentekoste, na ninyi watu, ati, mnaamini katika uponyaji wa Kiungu? Huyu hapa *nani* hapa, hebu niwaone mkimponya.”

⁸⁰ Huyu ni ibilisi yule yule wa kale, yeye yule aliyesema, “Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, yaamuru mawe haya yafanywe kuwa mkate.”

⁸¹ Ibilisi yule yule wa kale, wakati macho Yake yalifunikwa, walimpiga kichwani kwa fimbo, na kusema, “Sasa,” wakapitishiana fimbo, wenyewe kwa wenyewe, na kusema, “twambie ni nani aliyekupiga, nasi tutakuamini kama Wewe ni Nabii.” Kamwe hakujibu. Yeye hamfanyii vitimbi mtu yeyote. Naam.

⁸² Yeye yule, wakati alipokuwa msalabani, alisema, “Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, shuka msalabani na kuthibitisha ya kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu.” Angeweza kufanya hivyo.

⁸³ Wao walimpa sifa kubwa sana aliyopata kupewa, pale, lakini hawakujua. Walisema, “Aliwaokoa wengine; Yeye Mwenyewe hawezi kujiokoa.” Kama angejiokoa, asingeliweza kuwaokoa wengine. Yeye alijitoa kusudi aweze kuwaokoa wengine. Mnaona, Hawakuutambua Uwepo wa Mungu. Hivyo tu.

⁸⁴ Sasa huo unaachilia nguvu za uponyaji, na kitu gani? Utaachilia nguvu za kuyafungua macho yako yapate kumtambua, ama kuyafumba macho yako kusudi usiweze kumtambua kamwe. Kinachoyafungua macho ya mmoja, huyafumba macho ya asiyeamini.

⁸⁵ Lakini, ule mji, hawakuwa na imani yoyote Naye. Kwenye nyumba ya yule Mfarisayo, alimwalika aje; kwa Simoni, Mfarisayo, naye alikuwa amepika chakula kingi kitamu cha jioni, naye Mfarisayo alitaka kuwathibitishia Yeye hakuwa Nabii hata kidogo. Kwa hiyo alikuwa kule nyuma wakipongezana kwa glasi na bilauri zake, na manukato yote mazuri nyumbani.

⁸⁶ Na Yesu alikuwa ameingia akampita mtumishi mtawadha miguu, na alikuwa ameketi chini hapa. Na, mchafu, harufu mbaya ya—ya kondeni juu Yake, ambapo wanyama walikuwa wamepitia, na mavazi Yake. Hiyo ndiyo sababu waliosha miguu yao siku hizo.

⁸⁷ Na, mnaona, jambo la kwanza, unapoalikwa nyu—nyumbani huko Palestina, wakati walipovaa hayo makubadhi, jambo la kwanza walilofanya lilikuwa ni kuiosha miguu yako, kisha wanakupa kitu fulani; kutembea kwenye zulia zao, zile zulia nzuri sana za Uajemi na kadhalika, zilikuwa ni za kupendeza sana.

⁸⁸ Jambo la pili walilofanya, halafu walikupa mafuta mkononi mwako. Yanatokana na tofaa dogo linalopatikana huko juu sana mlimani, tofaa waridi. Baada ya waridi kwisha, linaacha tofaa na manukato mazuri. Nao wa—wanayasugulia usoni mwao. Na hiyo miali ya moja kwa moja ya jua la Palestina ni mibaya sana, na, unaona, hilo linaondoa harufu. Na—na halafu ukifanya hivyo, ndipo mwenyeji anakuja mlangoni na kuwabusu shingoni na kuwakaribisha.

⁸⁹ Hao watawadha miguu walimwachaje Yesu apite, bila ya kuiosha miguu Yake ama—ama—ama kumpa mafuta ya kujipaka, ama hata kumkaribisha kwa busu?

⁹⁰ Lakini kulikuwako na maskini kahaba mmoja mtaani. Hao wanadini wote wakiwa kule sasa, kundi hilo lote halikumtambua. Ndipo maskini mwanamke mwenye sifa mbaya, alichungulia mle, labda langoni, naye akamwona ameketi kama ua la ukutani.

⁹¹ Hivyo ndivyo alivyo siku hizi miongoni mwa kundi la dini pia, ua la ukutani, hakaribishwi, hatakiwi. “Kinyaa, mchafu, mtakatifu anayejifingirisha,” ndivyo wanavyomwita, “namna fulani ya m—mtu asiye na akili zake timamu; mpiga ramli, msoma mawazo,” ama namna fulani ya jina baya.

⁹² Na Yesu, nitalifikia katika dakika chache, akasema, “Ukisema neno dhidi ya Mwana wa Adamu, utasamehewa; bali Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya jambo lile lile, hutasamehewa hata neno moja.” Unaona?

⁹³ Lakini pale maskini mwanamke huyo aliona Yeye alihitaji kuhudumiwa. Ndipo akafanya hima, akaenda na kutwaa chupa ya marimari iliyojaa mafuta. Labda alikuwa ameinunua kwa fedha za kutokana na ukahaba wake. Lakini ilikuwa ni kitu gani? Huenda aliwazia, “Yeye ni—Yeye ni Nabii. Lakini ninakumbuka mwanamke mwingine mwenye matatizo kama yangu, mtu mwingine kama mimi; yeye alikuwa na nafasi na akamtambua Yeye, ndipo akasamehewa.” Huko juu kwenye kisima cha Sikari, jana usiku tulilizungumzia hilo. “Na kama ninaweza tu kumfikia, ninajua Yeye ni Nani, nitamtumikia. Kama hao wengine, sijali wanafanya nini. Nitamtumikia. Nitatambua ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu.”

⁹⁴ Akaingia haraka. Akamkaribia sana, naye akajisikia mwenye hatia sana. Hivyo ndivyo mwenye dhambi anayetubu halisi anavyojisikia katika Uwepo Wake, mwenye hatia!

⁹⁵ Ndipo machozi yakaanza kutiririka, naye alikuwa akijaribu kuyaficha. Yakaangukia miguuni Mwake. Alikuwa yuaenda kumtia mafuta, lakini machozi yanaanguka miguuni Mwake. Ndipo akaanza kuyapangusa, na—na kulia, na—na kuyapangusa kwa mikono yake. Na—na miguu Yake ilikuwa ikichafuka kwa uchafu iliyokuwa nao; na—na kama ukitaka kuliadini kweli, akiwa na harufu mbaya ya wanyama njiani, kila mtu alipitia njia iyo hiyo. Na ilikuwa hapo, harufu mbaya juu yake, ameketi pale, nayo machozi yake yalikuwa yakianguka miguuni Mwake, na yeye alikuwa akijaribu kuyapangusa. Na hakuwa na taulo.

⁹⁶ Uzuri wa mwanamke na heshima yake ni nini? Ni nywele zake. Hiyo ndiyo sababu wengi wenu ninyi wanawake siku hizi huzikata zote. Hilo ni kosa. Yeye, alizishika nywele zake na akaanza kuosha ninii. . . Miguu Yake, na kuipangusa, nywe—nywele zake nzuri, akimwondolea harufu mbaya, anaichukua

mwenyewe, akiichukua dhihaka Yake. Loo, jamani! Hapo ndipo unapotambua ni Nani aliye mbele zako. Unaona? Dada zetu ingewabidi karibu kusimama kwa kichwa chao, waweze kupata nywele za kutosha kufanya hivyo. Basi hapo akaiosha miguu Yake, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake, kisha akaibusu miguu Yake.

⁹⁷ Na maskini huyo Simoni akisimama pale nyuma, alisema, “A-ha! A-ha!” Loo, ninaweza tu kumwona akilipuka. Yeye hakutambua Huyo alikuwa ni Nani. Akasema, “Niliwaambia Yeye hakuwa ni Nabii. Angalikuwa ni Nabii, angalitambua ni mwanamke wa jinsi gani aliye karibu Naye.”

⁹⁸ Yesu kamwe hakusogeza mguu. Alimwangalia tu. Na mwanamke huyo alikuwa na woga.

⁹⁹ Ndipo baada ya kumaliza, yeye akimtumikia, aliangalia kule, akasema, “Simoni, nina jambo la kukwambia. Ulinialika hapa. Ulinileta hapa,” kwa maneno mengine, alikuwa anamtega. “Ulitaka kunianika. Ulitaka kuthibitisha ya kwamba sikuwa kile nilicho. Nawe, uliponileta hapa, ulipaswa kuhakikisha nimeoshwa miguu, bali hukufanya hivyo. Unapaswa kunipa mafuta ya kutia kichwani Mwangu, bali hukunipa. Hukuniaribisha kwa busu. Na mwanamke huyu, tangu nimekuwa hapa, ameitawadha miguu Yangu kwa machozi yake, na kuipangusa kwa—kwa nywele zake, na hajaacha kuibusu miguu Yangu tangu nimekuwa hapa. Nina neno dhidi yako, Simoni.”

¹⁰⁰ Halafu anamgeukia mwanamke. Ninaweza tu kuwazia kumwona amesimama pale, na macho yake makubwa marembo yote yamechafuka, na uso wake, na ambapo alikuwa na grisi na—na mavumbi ya barabarani, usoni mwake. Naye anawazia, “Sasa je! nimekosea? Nimekosea?”

¹⁰¹ Akasema, “Nami ninamwambia, ‘dhambi zake ambazo ni nyingi, zote zimesamehewa. Nenda kwa amani.’”

¹⁰² Ilikuwa ni kitu gani? Alitambua. Aliitambua nafasi yake. Unaona? Aliitambua. Alimtumikia. Mafarisayo hawakumtumikia. Aliuona na akautambua Uwepo Wake, nao ulifanya nini? Uliosha. Ulimfungulia nini? Msamaha. Ukamfungulia, msamaha wa dhambi zake. Ulifanya nini pia? Pia uliachilia nguvu za Mungu, kuwaonyesha hao wasioamini ya kwamba Yeye alikuwa ni Nabii. Yeye alijua mwanamke alikuwa ni nani. Pia ulifungulia furaha na nguvu na Uzima wa Milele. Uliufungulia huo.

¹⁰³ Lakini yule aliyesababisha msumari mkubwa mno kupigiliwa kwenye miguu hiyo ya thamani, yeye hakuutambua Uwepo wa Mungu ndani Yake. Yeye pia alitaka amfanyie kitimbi rahisi, burudani kidogo.

¹⁰⁴ Hicho ndicho ulimwengu unachopenda, siku hizi, ni lundo la burudani. Hauitaki Injili. Wanataka kutumbuizwa.

¹⁰⁵ Naye Pilato alisema, “Ningependa kutamani miujiza kutoka Kwake, ama kitu kama hicho. Mleteni hapa.” Moja kwa moja mbele za Mungu, na akamkataa, kwa sababu (gani?) yeye alipendezwa na—na maoni ya watu zaidi ya alivyopendezwa na ile fursa ya kuwa Mbele za Mungu. Ni jambo gani lililotukia? Yule mwanamke alisamehewa, na kupewa Uzima wa Milele; bali yeye alirukwa na akili akawa mwendawazimu, kisha akajiua kwa kujizamisha akafa maji huko Uswisi.

¹⁰⁶ Sasa, shughuli, alichukuliwa sana na maoni yanayopendwa na watu wa siku ile, kwamba, “Alikuwa ni Beelzebuli; alikuwa anajifanya tu kuamini; kwa kweli hakukuwa na chochote Kwake,” yeye, yeye alifanya nini? Aliipoteza, aliipoteza nafasi yake Mbele za Mungu. Angeweza kusamehewa. Yeye alisema, “Ninayo mamlaka ya kukusulibisha. Ninayo mamlaka ya kukufungua.”

¹⁰⁷ Akasema, “Huna mamlaka isipokuwa imetoka kwa Baba Yangu.” Alipaswa kujua, kama angeliyafahamu Maandiko. Naye, akiwa ni Myahudi, alipaswa kujua hilo. Lakini, unaona, mapokeo yalikuwa yamemfundisha vibaya. Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Laiti angelifundishwa vema! Laiti mtu huyo angeliamini yale Maandiko yalikuwa yamesema! Lakini mapokeo yake yalimwelekeza kwingine.

¹⁰⁸ Ndivyo ilivyo siku hizi. Watu wataichukua Injili halisi, ambapo Roho Mtakatifu anaingia, na nguvu na utukufu wa Mungu ukiwafungulia wenye dhambi na kuwafanya huru, na kuwabatiza katika Roho Mtakatifu, na kuwaponya wagonjwa, na kuonyesha ishara na maajabu, na watu wataondoka, wakisema, “Aha! Sasa unajua kile kanisa langu linachoamini? ‘Huo ni upuuzi!’” Unaona, unapoteza, unauza haki zako za mzaliwa wa kwanza. Esau mwingine!

¹⁰⁹ Wengi sana hupata nafasi ile ile siku hizi, kusimama katika Uwepo Wake kama walivyofanya wakati huo. Na bado, kwa sababu ya maoni ya watu wengi, wanaikataa. Wakisimama katika Uwepo wa Mungu! Sijui, rafiki, usiku wa leo, kama sisi watu tulio Wakristo, katika Uwepo Wake, na tu wagonjwa, kama hatuikatai nafasi ya kuponywa kwa kumwamini Yeye tu? Sisi ambao tunadai kumwamini Yeye, kweli hatuutambui Uwepo Wake, kile alichohidi kufanya leo.

¹¹⁰ Akithibitishwa na ahadi ya siku ile, Yesu alikuwa akikikemea kizazi hicho kwa kutokuamini ishara Yake ya Masihi. Tunaiona hapa, Yeye alikuwa akiwakemea. Wakimwita Beelzebuli! Walimtaka afanye ishara ya Musa, labda, aifungue Bahari ya Shamu. Walimtaka afanye ishara ya Daudi, kukichukua kiti cha enzi na serikali. Lakini hakuna Andiko lililosema ya kwamba angefanya hivyo. Alikuwa awe Nabii. Yuaja, Mfalme. Alikuwa awe Nabii wakati huo, Naye alifanya ile ishara ambayo Mungu alisema angeifanya katika siku

hizo, nao wangali walikuwa wakitaka afanye ishara fulani iliyowapendeza. Mnaona?

¹¹¹ Nami tu nashangaa kama hatuungalii huko mbele sana kuona kitu kilicho papa hapa karibu nasi. Nashangaa kama ingeweza kuwa vivyo hivyo, kama tungeipita nafasi yetu? Kumbukeni, kama ilivyokuwa mifano ya kale, mifano kamwe haiwezi kushindwa. Ishara ya mwisho, kulingana na Yesu, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika siku ambapo Mwana wa Adamu,” sio Mwana wa Mungu sasa, “atakapofunuliwa Mwana wa Adamu.” Angalieni hapa mahali lilipo leo! Enyi marafiki, ningeweza kuwaambia mambo hapa ambayo si vizuri kwangu kuwaambia, bali yangewashangaza sana.

¹¹² Ninataka kuwaulizeni swali dogo tunapomalizia, kabla hatujaendelea na ibada hii, dakika chache tu. Sijui kama ningeweza kuwauliza hili.

¹¹³ Mtu yeyote anajua ya kwamba ulimwengu, mahali ulipo, kila kitu kiko katika utaratibu wa Kuja Kwake. “Matetemeko ya nchi mahalimahali; mwezi unatema damu nyekundu, ama volkano nyekundu kila mahali, zikiufunika,” kama vile Yesu alivyosema tuiangalie ishara hiyo katika siku za mwisho; “bahari ikivuma, watu wakivunjika mioyo kwa hofu, na mshangao wa wakati, dhiki miongoni mwa mataifa.”

¹¹⁴ Angalieni upotovu unaoendelea leo! Uangalieni leo, ongezeko la asilimia arobaini California, la walawiti, mapenzi asilia ya kimwili yamekwisha potea.

¹¹⁵ Hebu angalieni kwenye... Angalieni leo, jinsi ambavyo watu watakaa nyumbani, wanaojiita Wakristo, na kuwasikiliza watu kama Pat Boone, Elvis Presley, Ernie Ford, na hao wanaoimba nyimbo za dini Jumapili; na kuangalia vitu hivyo, wanawaangalia wakiwabusu hao wanawake, na kadhalika huko nje.

¹¹⁶ Wakati, hakuna mtu anayepaswa kumbusu mwanamke mpaka awe amemwoa. Hizo ni tezi za kiume na za kike zikikutana. Acha iwe popote pale, ni kosa. Kimsingi ni tendo la kujuana kimwili. Wakati tezi za kiume na za kike zinapogusana, ni tendo la kujuana kimwili. Na limefanywa... Mwanamume akimbusu mwanamume mdomoni, lingemfanya atapike, ama mwanamke mwanamke. Ni kwa nini ni tofauti? Ni ninii—ni tendo la kujuana kimwili, kimsingi. Hiyo ni kweli. Mfano wa Kristo akimbusu Bibi-arusi Wake, mnaona. Hupaswi kufanya hivyo kamwe.

¹¹⁷ Lakini angalia jambo hilo leo, sinema hizi zote na kadhalika, na lundo moja kubwa la kubusiana na kukumbatiana. Na karibu ni uzinzi wa hadharani kabisa, kila mahali, nao watu ni vipofu sana hawalioni. Kweli! Kila kitu kiko katika hali ya Sodoma, Wasodoma kila mahali, kama Biblia ilivyosema.

¹¹⁸ Mambo mengi sana, angalieni siku hizi, kile alichosema kingetukia! Angalieni zile ahadi alizofanya, zitakazotimia siku hizi. Halafu chunguza jambo hilo, kile kinachoendelea, uone mahali tulipo, ndipo uone kama Yeye angali katika Neno Lake ama la.

¹¹⁹ Walitaka kuona ishara ya Musa, ishara ya Daudi. Hiyo haikuwa ni kwa ajili ya wakati wao; iliahidiwa kwa ajili ya wakati wa Musa na nyakati hizo. Ahadi ya wakati huu haina budi kutimia. Alikuwa tayari amewaonyesha dhahiri, Yeye, kwa Maandiko, na akawaalika wakayachunguze Maandiko, wapate kuona ni siku gani waliyokuwa wakiishi.

¹²⁰ Anafanya jambo lile lile kabisa sasa hivi! Yachunguzeni Maandiko, ninyi mnaoiamini Biblia. Ni kitu gani kinachopaswa kutukia papa hapa kabla ya Kuja Kwake?

¹²¹ Uangalieni ulimwengu, katika mahali ulipo; sasa, huo ni ulimwengu. Liangalieni kanisa, mahali lilipo. Angalia mahali lilipo, “likianguka, vuguvugu, Laodikia, likiliondoa Neno.” Kitu hicho chote kinaingia katika baraza kuu la makanisa, Baraza la Makanisa Ulimwenguni, likiifanya ile alama ya mnyama; ambayo Biblia inatangaza kwamba ni kosefu, na mambo hayo yote, na hata hivyo Waprotestanti wanaelekea moja kwa moja mle ndani, kabisa, kwa kutokuyafahamu Maandiko. Mapokeo yao! Loo, wanataka m—m—m—mtu mwenye mamlaka, nao watampata. Watahakikisha wanampata.

¹²² Yeye alikuwa, angalieni, bali Yesu alikuwa amejitangaza Mwenyewe kwamba alikuwa ni Nani hasa, na alikuwa amewathibitishia kwamba Yeye alikuwa ni Nani, katika wakati Wake.

¹²³ Na ni jambo lile lile leo! Sasa hebu liangalieni, hebu tuchukue msingi huo wa Luka 17, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.” Uangalieni ulimwengu, liangalieni kanisa, hali ya Sodoma! Angalieni mahali alipokuwa Lutu; wakati watu hao hata walijaribu ku—walijaribu kuusukuma mlango, wawapate malaika hawa, wanaume hawa.

¹²⁴ Angalieni, angalieni hapa. Kumekuwako... Angalieni, Ibrahimu alikuwa huko juu mlimani. Hakuwa Sodoma. Huo ni mfano.

¹²⁵ Daima kuna matabaka matatu ya watu katika kusanyiko la dini; waaminio, wanaojifanya waaminio, na wasioamini. Ni hao watatu sikuzote! Na hao hapo; kuna Wasodoma wasioamini, Lutu anayejifanya mwaminio, na Ibrahimu kanisa teule.

¹²⁶ Sasa, angalieni wajumbe wao katika siku ile. Wajumbe wawili walishuka wakaenda wakahubiri Sodoma. Hawakufanya miujiza yoyote, ila tu waliwapiga kwa upofu. Kuhubiriwa kwa Neno hufanya hivyo.

¹²⁷ Lakini angalieni ni muujiza wa aina gani Malaika huyu alifanya ambaye alibaki na Ibrahimu. Alikuwa ameugeuza mgongo Wake. Na akamwambia Ibrahimu jina lake lilikuwa limebadilishwa; akamwita "Ibrahimu" badala ya Abram. Asingepata yule mtoto mpaka jina lake lilipobadilishwa, wala Sara. Aliwaambia jina lao lilikuwa ni nani. Malaika aliwaambia hilo. Naye akasema kwamba atamzuru Sara majira kama hayo mwakani.

¹²⁸ Ndipo Sara akacheka kuhusu jambo hilo. Na Sara alipocheka... Huyu Mtu akiwa ameugeuza mgongo wake, Mtu huyo akila nyama ya ndama, na kunywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, na akila mkate; Mtu, mavyumbi nguoni Mwake, msafiri, alikuwa ni Mungu Mwenyewe. Na Ibrahimu akatambua jambo hilo kwa sababu Huyu alijua mawazo yaliyokuwa katika moyo wa Sara nyuma Yake. Kasema, "Kwa nini Sara alisema moyoni, 'Mambo haya yanawezekanaje?' Kuna jambo lililo gumu sana kwa Mungu?" Mnaona? Ndipo Sara akatoka nje upesi na kulikana. Akasema, "Naam, lakini ulicheka." Sasa, Yeye angaliutwaa uhai wa Sara papo hapo, kwa yeye kutokuamini, lakini, unaona, yeye ni sehemu ya Ibrahimu.

¹²⁹ Na kutokuamini kwetu katika dhihirisho Lake kuu katika saa hii; sisi ni sehemu ya Kristo. Yeye ananinii tu, unaona, sisi ni—sisi ni, unaona, ninii yetu... Yeye—Yeye hana budi kulitimiza.

¹³⁰ Sasa, angalieni, hakujakuwako na wakati katika historia ya wakati wa kanisa... Nami ninamjua mwanafunzi mmoja halisi ninayesema naye, mwanahistoria. Hapajapata kuwapo. Ningemwuliza mwanafunzi yeyote wa Biblia kuniambia mtu mmoja ambaye alipata kutumwa katika wakati wa kanisa, katika kanisa hili tangu kule kusulibishwa kwa Kristo, huduma ya ulimwenguni kote, ambaye jina lake lilipata kuishia katika h-a-m, kama vile A-b-r-a-h-a-m, mpaka siku hii. Sankey, Finney, Moody, Knox, Calvin; lakini popote palipokuwa na G-r-a-h-a-m hapo kabla, Billy Graham, yule mwinjilisti mkuu huko hudumani pamoja na madhehebu yaliyoko huko Sodoma? La hashu. Kuna Oral Roberts wa kisasa huko nje pamoja na Wapentekoste, jambo lile lile. Je! mlijua jambo hilo?

¹³¹ Lakini, h-a-m! Sasa, G-r-a-h-a-m ni herufi sita tu, bali A-b-r-a-h-a-m ni herufi saba. Sita ni namba ya mwanadamu, shirika la mwanadamu, kazi ya mwanadamu; bali A-b-r-a-h-a-m ni herufi saba. Sasa angalia, katika Kanisa teule ambalo limetolewa, si hayo madhehebu, bali kanisa teule litakaloonekana wazi, linapaswa kupokea mjumbe, pia, katika siku za mwisho.

¹³² Ni kitu gani kinachoendelea huko chini? Ni kitu gani kinachoendelea huku juu? Linganisha hilo na lile Yesu alilosema. Kamwe katika historia hatujapata kuketi namna hii. Na ishara

zile zile ambazo zingefanywa! Hivi hamtambui, enyi marafiki, na kutambua kwamba ni Mungu ameshuka katika Injili, katika watu Wake, akijitambulisha Mwenyewe? Hivi hamwezi kuitambua saa tunayoishi? Hivi tumefikia tu kwenye kupiga makofi kidogo, kucheza piano, na kukariri *hili*, na—na kuliacha Neno, mpaka tumekuwa vipofu sana kwake? Hakika sivyo tulivyo. Hebu na tuitambue saa tunayoishi.

¹³³ Petro, Nathani, ama Nathanaeli, hasa, na yule mwanamke, waliitambua. Wao, wao—wao waliitambua ishara Yake, ishara ya Masihi.

¹³⁴ Ni vile vile sasa kama mambo haya ninayosema. Halafu kwa wakati huu, Yesu alisema. . . Sasa angalieni, Yeye anarejea nyuma sasa, akiwaambia juu ya wakati fulani. Mungu, katika wakati wowote, wakati alipoutuma Ujumbe Wake, ambao ulikuwa ni Neno Lake, na kulitambua kwa wakati huo; watu waliouamini, ulikuwa ni wakati mkuu kwao; watu ambao hawakuuamini, waliingia katika machafuko. Daima imekuwa hivyo.

¹³⁵ Kama vile katika siku za Yesu, jambo lile lile. Mwangelie akisimama hapa sasa. Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Yona, katika Yona; kwani kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi, siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo ndivyo itakavyokuwa na Mwana wa Adamu.”

¹³⁶ Yeye alisema, “Kizazi kiovu na cha zinaa kitatafuta ishara.” Sasa mnajua kile ninachofikiri alikuwa akifanya? Alikuwa akitabiri, “Kizazi kiovu na cha zinaa.”

¹³⁷ Sijui kama mtu yeyote aliye na akili timamu angeweza kukana kwamba hatuishi katika kizazi dhaifu na cha zinaa, wakati walawiti, upotovu! Na kiasi cha talaka Marekani kiko juu zaidi kuliko taifa lingine lolote ulimwenguni. Na ulimwengu mzima umeingia katika machafuko yake. Watatu kutoka kwa kila wanne, karibu hivyo, wametaliqiwa; kote, tukichukua jambo hilo lote katika miaka kumi ya ndoa. Mnaona? Wazieni jambo hilo! Talaka, kuoa tena na kuoa tena, kotaliki na kuoa tena. “Walikuwa wakila, wakinywa, wakioa wake na kuolewa.” Angalieni saa tunayoishi. Ni lini ulipowahi kuwa katika machafuko kama haya?

¹³⁸ “Kizazi kiovu na cha zinaa kitatafuta ishara, angalieni, nao watapata ishara.” Ati nini? Kizazi hiki. “Kwani kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi, siku tatu mchana na usiku, Mwana wa Adamu hana budi kuwa katika moyo wa nchi siku tatu mchana na usiku.” Ni ishara gani kizazi hicho kiovu na cha zinaa kitapokea? Ishara ya kufufuka.

¹³⁹ Na siku hizi, baada ya miaka elfu mbili, tungali tunamwona Yesu Kristo katika nguvu za kufufuka Kwake, akisimama miongoni mwetu, akifanya mambo aliyofanya wakati huo na alioahidi kufanya. “Kizazi kiovu na cha zinaa kitatafuta ishara,

sikuzote kikitaka ‘nionyeshe *hili*, na kama unaweza kufanya *hili* na kufanya *hili*.’ Wataipata, ile ishara ya kufufuka.” Ni yeye yule jana, leo, na hata milele; Neno lililodhihirishwa, likiishi miongoni mwetu. Jinsi tunavyopaswa kumshukuru Mungu kwa ajili ya ishara Yake kuu!

¹⁴⁰ Angalieni Yeye alirejea kwenye jambo lingine pale. Yeye alisema, “Na kama vile malkia wa kusini atakavyosimama,” huyo ni malkia wa Sheba. Sikilizeni kwa makini sasa.

Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki; naye atawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

¹⁴¹ Angalieni, hebu turejee kwenye hilo, dakika chache. Yeye alikuwa akisoma Biblia ile ile tunayosoma, kuhusu Yona, pia alikuwa akisoma kuhusu Sulemani. Sasa, wakati wa Sulemani ulipoanza, yeye alikuwa na . . . alikuwa na karama ya utambuzi. Na watu wote, taifa zima, waliamini. Kila mmoja alikuwa na moyo mmoja na nia moja. Kila mtu aliiamini.

¹⁴² Kama kila mtu, usiku wa leo, kama Marekani nzima, wangemrudia tu Mungu na kumwamini Mungu, hiyo ndiyo dhamana iliyo bora zaidi tuliyo nayo, itakuwa ndiyo ngome zote za kujisetiri na mabomu na chochote kile.

¹⁴³ Hakuna mtu aliyemchezea Sulemani. Walimwogopa kwa sababu alikuwa ni mtu mwenye kipawa. Nao watu walimwamini hivyo, alitumwa kutoka kwa Mungu, mpaka wakamfanya mfalme wao. Mataifa yote yaliwaogopa; si kwa sababu ya nguvu zao za kijeshi, bali kwa sababu Mungu alikuwa pamoja nao.

¹⁴⁴ Na kama taifa hili linalodai kwamba ni la Kikristo, kama lingeninii tu, wote kwa pamoja, waikumbatie karama hii kubwa ambayo tumepewa katika siku hizi za mwisho, Roho Mtakatifu wa Mungu juu ya Kanisa. Sio kanuni za imani. Roho wa Mungu! “Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali kwa Roho Yangu,” asema Mungu. Roho Mtakatifu, Yesu Kristo katika umbo la Roho, juu yetu, “yeye yule jana, leo, na hata milele,” akilifanya Neno hili liishi kile alichosema lingeishi. Angalieni kwa makini sasa.

¹⁴⁵ Loo, habari zilisambaa kote ulimwenguni! Hawakuwa na televisheni na redio, na kadhalika siku hizo, kwa hiyo zilisambazwa toka mdomo hadi sikio. Ndipo baada ya kitambo kidogo ule msafara mkubwa ukashuka ukaja kupitia Jangwa la Sahara, ambayo ni safari ya miezi mitatu kutoka Palestina kufikia mahali huyo malkia alipoishi. Nayo imani chanzo chake ni (kitu gani?) kusikia, kusikia Neno la Mungu. Naye alikuwa amesikia juu ya mkutano huu mkubwa waliokuwa nao kule, na wakati wowote msafara ulipokuja kutoka huko, angeuliza, “Je! mmeninii, mmepitia Palestina?”

“Naam.”

“Loo, vipi kuhusu jambo hilo?”

146 “Loo, ni—ni zaidi ya chochote kile! Kamwe hujapata kuona utambuzi kama huo. Na ni kama tu mungu mdogo ameketi pale. Mungu wao amewakilishwa katika mtu aitwaye Sulemani.”

147 Vema, “imani chanzo chake ni kusikia.” Maskini moyo wa malkia huyo ukaanza kuona njaa ya kukwea kwenda kule na kujionea mwenyewe. Mnaona, alikuwa amekusudiwa Uzima.

148 Angalia sasa, jambo la kwanza la kufanya sasa, yeye akiwa ni kafiri, ilimbidi kwenda kuomba ruhusa kutoka kwa kuhani wake, ili kwenda. Kwa hiyo naweza kuwazia nikimwona akimwendea kuhani wake, na kusema, “Baba mtakatifu, ninasikia wana uamsho mkuu huko Pa—Palestina. Ningependa nipate ruhusa nipande niende na nikajionee mwenyewe.”

149 “Sasa, mtoto wangu, sasa hutaki kujichanganya katika ninii. . . Hata hivyo, hatushiriki katika uamsho huo, kwa hiyo wewe—wewe huwezi kwenda. Unaona, hilo ni lundo tu la upuuzi. Hakuna—hakuna kitu hapo. Hao watu wanadai wamepitia kwenye Bahari ya Shamu, na ati wamefanya *yote haya, yale*. Hakuna kitu hapo. Kama kungekuwako na chochote kama hicho kikitukia, kingekuwa ni papa hapa kanisani petu.” Tungali tuna wapagani.

150 Kwa hiyo tunaona ya kwamba alianza kuona njaa. Akasema, “Sasa angalia,” akasema, “wananiambia, ya kwamba ‘Mungu wao kule juu amewakilishwa katika mwanadamu, na hekima yake imepita chochote kile. Utambuzi wake ni wa ajabu sana.’”

“Loo, hakuna kitu hapo.”

Huyo malkia akasema, “Lakini huenda ni—nikaninii. . .”

151 “Vema, angalia, wewe ni malkia, huwezi kuhusishwa katika kundi kama hilo la watu. Hilo, huwezi kufanya hivyo. Kundi hilo la watu, linalojulikana ulimwenguni kote kama walokole wa dini. Huwezi kufanya hivyo.”

152 Lakini, unaona, Mungu anapoanza kuushughulikia moyo wa mwanadamu, hakuna kitu kitakachouzuia. Mume, mke, watoto, mchungaji, hakuna kitu kingine chochote kinachoweza kuuzuia wakati mtu anapomwonea Mungu njaa. Watashika njia, kwa vyovyote vile. Kwa hiyo akawa tayari, kujiandaa.

153 Vema, yeye angesema, “Vema, nitakupa tu. . . Ita—itabidi kukufukuza kutoka kwenye ushirika wetu.”

154 “Vema, unaweza tu kufanya hivyo. Ninaenda, haidhuru. Ninaenda kulichunguza mwenyewe jambo hili, na kujionea.”

155 Alikuwa amekuja na magombo na alikuwa amesoma kile ambacho Yehova anapaswa kuwa, juu ya manabii Wake na kile anachopaswa kufanya, jinsi ambavyo Neno la Mungu lingedhihirishwa, jinsi lingeyajua mambo haya wakati

lilipowakilishwa, likifichwa katika mwili wa binadamu, kile lingefanya. Naye alikuwa ameyasoma mambo haya yote.

Kwa hiyo ningemsikia kuhani akisema, “Vema, angalia, kitabu chetu kinasema *hivi*,” akasema.

¹⁵⁶ “Naam, angalia, mimi. . . nyanya wa nyanya wa nyanya wa nyanya yangu alisimama mbele ya sanamu zizo hizo. Alisimama na kukariri sala, siku baada ya siku. Kamwe hapakuwapo na msogeo hata mmoja, mnong’ono, wala chochote kile. Nami nimechoka, maskini umbo hili la kale mfu. Ninataka kuondoka niende nikaone kama kuna Mungu aliye hai.” Ni vibaya sana hatuna wengi zaidi wa hao malkia siku hizi.

¹⁵⁷ Kwa hiyo akajiandaa kuondoka. Sasa wakati alipofikia mahali hapa ambapo hana budi kwenda, sasa, kumbukeni, alikuwa na shida kubwa. Haikuwa rahisi jinsi ingalikuwa kwenu. Sasa angalieni kile kilichombidi kufanya.

¹⁵⁸ Hili hapa jambo lingine ninalotaka, sitaki kuliacha. Yeye alisema hivi, “Ninapanda kwenda kule, nami nitabeba kiasi fulani cha pesa. Nitachukua zawadi. Na kama ni kweli, nitaliunga mkono. Kama si kweli, basi ninaweza kurudi na pesa zangu.”

¹⁵⁹ Mwanamke huyo angeweza kuwafundisha Wapentekoste. Naam, bwana. Kuunga mkono vitu huko nje vinavyocheka na kudhihaki uponyaji wa Kiungu, na hata hivyo mnaunga mkono vipindi vya redio badala ya kanisa lenu wenyewe, hiyo ni kweli, na vinacheka na kudhihaki mambo yale hasa mnaoamini.

¹⁶⁰ Lakini alisema, “Nitazichukua. Na kama si kweli, ninaweza kuzirudisha.”

¹⁶¹ Sasa kumbukeni, pamoja na mali hii yote pale, kwenye ngamia hawa. Na sasa kumbukeni, makundi ya wapanda farasi wa Ishmaeli waliokuwa ni maharamia wa jangwani, walikuwa kule. Lingekuwa ni jambo rahisi jinsi gani kwao kuyavamia ma—mawindo haya, na, mbona, wangewaua wale matowashi wachache waliokuwa pamoja naye, na kuwanyang’anya hizo fedha na kwenda zao.

¹⁶² Lakini kuna kitu fulani juu ya jambo hilo, wakati kweli umeyakinia, na Mungu anajifunua, umeyakinia kumwona Kristo, hakuna hatari mbele zako. Hata hujali chochote! Daktari anasema utakufa, hata hulioni hilo. Wakati unaposihi sana, unajua kuna jambo fulani pale.

¹⁶³ Kitu fulani ndani ya moyo wake, kikiwaka moto, imani katika Mungu huyu! [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . miezi mitatu ya kuvuka Jangwa la Sahara. Sio kwenye Kadilaki iliyoyoyozwa. La, la. Alichukua miezi mitatu kulivuka Jangwa la Sahara, labda akisafiri usiku, akiyasoma yale magombo, kwenye oasisi mchana, mpaka alipofika.

164 Sasa, si ajabu Yesu alisema huyo atasimama katika siku za mwisho na kukikuhumu kizazi hiki, kwa kuwa baadhi yao hawatavuka barabara; na aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa, Roho Mtakatifu Mwenyewe. Mnaona? Si ajabu atasimama katika siku za mwisho na kukihukumu kizazi hiki!

165 Angalia, hatimaye aliwasili. Yeye hakuja kama watu wengi, watu wengine watakuja kwenye mkutano wa ajabuaajabu. Alikuwa na akawachukua ngamia wake, na akaingia uani, akapiga hema zake, naye alikuwa akae hapo mpaka atakaposhawishika.

166 Watu wengi sana watakuja, waketi labda dakika tano, labda ishirini na tano. Mara huyo mwinjilisti ama mtu fulani akisema jambo fulani ambalo ni kinyume na yale mwanamke huyo a—anawazia kwamba kanuni zake za imani zinayosema, ama mwanamke, kanuni za imani za mwanamume huyo, hao wanaondoka. Mnaona, hata hawana adabu. Si ajabu atakihukumu kizazi hiki; yeye alikuja kukaa mpaka ashawishike.

167 Ninaweza kuwazia ibada ya kwanza asubuhi hiyo, wakati parapanda zote zilipolia, Mchungaji Sulemani alitoka. Huenda malkia alikuwa ameketi huko nyuma kabisa. Akasema, “Sasa nitajionea mwenyewe. Ninajua hivyo ndivyo Yehova anavyopaswa kuwa. Mwanadamu anaweza kufanya madai, bali nitaona.” Kwa hiyo akaketi pale siku hiyo na kuangalia, naye akaona kila mtu akija jukwaani. Akaona kwamba utambuzi huo ulikuwa ni mkamilifu.

168 Hatimaye, hebu tuseme kadi yake ya maombi iliitwa, ambayo labda haikuitwa, bali wakati wake uliwadia wa kuja mbele ya Sulemani. Nayo Biblia ilisema, ya kwamba, “Wakati alipokuja kusimama mbele ya Sulemani, ya kwamba Mungu alimjaliza Sulemani kujua siri zake zote. Hakukuwako na chochote kilichofichika.” Basi mwujiza ukafanywa juu yake.

169 Ndipo akawageukia wasikilizaji, na kusema, “Mambo haya yote niliyosikia ni ya kweli, na hata ni makuu kuliko niliyosikia habari zake.” Unaona? Loo, roho yake ikazimia, akashindwa kupumua, kwa maana huyu hapa mtu asiyemjua, mgeni, ameyafunua mambo aliyotaka kujua.

170 Loo, na Yesu akisimama pale, ambaye alikuwa ni zaidi ya Sulemani! Yeye alikuwa ni utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu aliyezaliwa na bikira. Alimfunika Yeye, na Yehova Mwenyewe akadhihirishwa katika mwili. Naye huyu hapa amesimama pale katika utimilifu, nao walisema wasingemwamini, utambuzi wa juu zaidi. Unaona, Yeye alikuwa ni Sulemani pamoja na Daudi, pamoja na hao wengine wote walikuwa wote ndani Yake. Manabii wote walijumuika katika Yeye, mkuu kuliko Sulemani.

¹⁷¹ Na hata katika siku hiyo, Yeye alisema, “Kama mkinena maneno hayo dhidi Yangu, nitawasamehe. Lakini ajapo Roho Mtakatifu, litakuwa ni jambo kuu kuliko lilivyo sasa, na hukumu zaidi.”

¹⁷² Na hapa tumesimama leo tukimwona Mungu yeye yule akifanya jambo lilo hilo! Ninaamini yeye atasimama kwenye Siku ya Hukumu na kukihukumu kizazi hiki, maana alitubu na kuamini ujumbe ambao Sulemani alikuwa akihubiri, na akamwamini Mungu. Aliona jambo lililo halisi.

¹⁷³ Unajua, shida ya leo, kuna watu, watu wengi, pamoja na watu ambao ni washiriki na wanaenda tu kanisani na kuwa na kanuni za imani. Mnaona, wameona mengi sana ambayo ni ya uongo, mengi sana ambayo ni sanamu tu, na wingi wa majengo makubwa mazuri. Na—na, sisi, hebu tusininii—hebu kamwe tusingie kwenye hamaki ya namna hiyo. Mnaona, Mungu haishi katika majengo makubwa; Yeye huishi moyoni mwako. Unaona, Mungu haishi katika elimu ya kiakili; yuko mbali sana nayo. Yeye huishi katika unyenyekevu, moyoni mwako.

¹⁷⁴ Yeye huishi katika Neno Lake, na Neno Lake huingia moyoni mwako na kujinenea, na kutangaza. Yeye hulifasiri Neno Lake Mwenyewe kupitia kwako. Yeye anajaribu kumpata mtu fulani ambaye anaweza kumshika, apate kuonyesha ya kwamba Yeye angali ni Mungu. Unaona? Na ndivyo alivyo, Yeye atafanya hivyo endapo tu anaweza kumpata mtu fulani anayeweza kumzungumzia. Kama anaweza kupata mwanamke mwingine anayetokwa na damu, angali anaweza kunena jambo lile lile. Angali anaweza kufanya jambo lile lile, akitambulisha, akitangaza. Tuko kwenye Uwepo wa Mungu, tusiutambue.

¹⁷⁵ Inanikumbusha juu ya hadithi ndogo. Huenda niliwhadithia hiyo wakati mmoja, sijui. Ingefaa sasa hivi. Kama nyote mjuavyo, mimi—mimi huwinda wanyama wakubwa. Nami nilikuwa huko kwenye misitu ya kaskazini, nilizoea kwenda huko kuwinda, wakati wote. Nami nilikuwa na rafiki huko jina lake Bert Call. Alikuwa ni mwindaji hodari, karibu ni nusu Mhindi. Haikukubidi kuwa na wasiwasi kumhusu, asingeweza kupotea. Nasi kweli tulikuwa marafiki wasiri, bali huyo alikuwa ndiye mtu katili kuliko wote, moyoni, niliyepata kumwona. Ni kwamba tu hakuwa na huruma hata kidogo. Alizoea kuwapiga risasi paa wadogo, hao ni watoto wa paa, ili tu kunifanya nijisikie vibaya. Naye angesema, “Loo, ninyi wahubiri ni waoga. Billy, wewe ungekuwa mwindaji mzuri kama usingekuwa mhubiri.” Kasema, “Wewe ni mwoga kupindukia.”

Nikasema, “Bert, huko si kuwa mwoga.”

¹⁷⁶ Sasa, ni sawa kuwaua wototo wa paa kama sheria inasema hivyo. Ibrahimu alimwua ndama na kumlisha huyo Mungu. Si ukubwa wake wala jinsia yake.

¹⁷⁷ Lakini ni uovu unaoambatana nalo, naye angewapiga tu risasi hao watoto wa paa kisha anachekeka tu, aangue kicheko kwa sababu jambo hilo liliniudhi. Vema, sasa, yeye—yeye alifanya jambo hilo.

¹⁷⁸ Basi mwaka mmoja nilipanda nikaenda kule. Naye alikuwa amejibunia filimbi ndogo ambayo angeweza kuipiga, kama mtoto mdogo wa paa, jinsi amwitavyo, mwajua, mama yake. Na kwa hiyo akasema, “Aisee, Billy, kabla hatujaanza asubuhi ya leo,” kasema, “ninataka kukuonyesha kitu fulani nilicho nacho.” Ndipo akanionyesha hiyo.

Nikasema, “Bert, kweli hutathubutu kutumia kitu kama hicho.”

¹⁷⁹ Akasema, “Loo, jirudie.” Naye jamaa huyo alikuwa na macho kama tu ya mjusi, kama vile baadhi ya wanawake hawa wanavyojaribu kuyapaka rangi macho yao, mwajua vipi, namna hiyo. Mnajua, akaniangalia, kwa hayo macho yaliyoonekana kama ya mjusi, na jicho, karibu liniogopeshe.

Ndi—ndipo nikasema, “Bert, usifanye hivyo.”

Akasema, “Loo, enyi wahubiri waoga!”

¹⁸⁰ Kwa hiyo tu—tulikuwa... Nilikuwa nimechelewa kidogo kuamka wakati huo. Na hao mikiamyeupe wa kaskazini... Kulungu wenu hapa wa nyumbu, atakukaribia, bali si mmoja wa hao jamaa. Wakati wowote anaporushiwa risasi, yeye ni ninii... Mwanena kwamba Houdini ni mwanasanaa mtoro, huyo ni kama mchezo, kwa hao. Kwa hiyo tulikuwa tumechelewa na walikuwa wamerushiwa risasi. Nao hao kulungu walikuwa wamejificha, wakila usiku kwenye mbalamwezi, na kulala mchana. Tulitembea umbali wote mpaka Kijinjia cha kale cha Jefferson, moja kwa moja mpaka juu ya Mlima Washington. Kulikuwa, kulikuwa na kama ichi sita za theluji ardhini, hali nzuri ya hewa ya kuwafuatilia wanyama; hatukuona mburuzo hata mmoja.

Akasema, “Unaonaje, Billy?”

¹⁸¹ Nikasema, “Hapo ninyi nyote mliwaogopesha wote wakatoroka sehemu hizi, kwa hizo bombomu mnazorusha.”

¹⁸² Na kwa hiyo tukaendelea. Baada ya kitambo kidogo, karibu saa tano. Sikuzote tulibeba moja ya hizo the—themosi ndogo iliyojaa chokoleti moto. Ni kwamba ukijeruhiwa, ama kitu kama hicho, hiyo ni kichangamsho, na sandwichi. Kwa hiyo ilikuwa ni kama saa tano ama saa tano na nusu, nadhani, tulipofika mahali pa wazi yapata ukubwa wa uwanja huu wa maonyesho hapa, ama jengo hili, wala hapana miti. Kwa hiyo kwa namna fulani aliketi tu chini, akaiegeza bunduki yake mtini, akaanza kuunyosha mkono wake *hapa* nyuma. Nami nilifikiri alikuwa akienda nyuma kuchukua ninii yake—kuchukua themosi yake. Nikafikiri, “Vema, tutakula.”

183 Kwa kawaida tunapanda juu ya mlima na kula, ndipo mmoja anaenda njia moja na mwingine njia nyingine, halafu tunarudi. Nasi tulijua njia za huko, vizuri. Na kama tungalipata kulungu, tulimtundika juu tu, kisha tunajua, tukaenda na kusaidiana kuwaleta ndani. Kwa hiyo nilidhani alikuwa tu akitaka kula chakula chake cha mchana, ndipo tungeachana, maana ilikuwa ni karibu tu mwisho wa msitu. Kwa hiyo mimi. . .

184 Akanyosha mkono nyuma. Nami nikaanza kutoa themosi yangu, nichukue chokoleti yangu, na nikaanza kuivuta hivyo. Ndipo akatoa ile filimbi ndogo mfukoni mwake, naye akaipiga kwa nguvu jinsi *hiyo*. Kisha akaniangalia kwa macho hayo kama ya mjusi tena, na kuipuliza filimbi hiyo. Basi alipoipiga, umbali tu kama wa jengo hili, kulungu jike mkubwa mno akasimama.

185 Sasa kama baadhi ya dada zetu huenda wasijue, kulungu jike ni mama kulungu. Na, mnaona, filimbi hiyo ilikuwa ni mtoto, naye alilia, ndipo mama huyu mkubwa akasimama. Na ni kama saa tano mchana, mtu yeyote anayewawinda kulungu anajua ya kwamba huo ni wakati mbaya. Wamelala.

186 Kwa hiyo alisimama akaangalia kotekote. Ningeweza kumwona vizuri sana. Aligeuka akaniangalia, akaipiga tena. Na badala ya—ya kutoroka, alikuja moja kwa moja kwenye uwazi.

187 Sasa, hilo si jambo la kawaida. Hawatafanya hivyo. Mwindaji yeyote anajua hivyo. Nao hawatatokea, wala hawatafanya hivyo. Lakini alitoka akaja moja kwa moja pale. Kwa nini? Yeye alikuwa ni mama; huyo alikuwa ni mtoto. Alikuwa, mnaona, amezaliwa tu ndani yake awe mama, na huyo ni mtoto.

188 Ndipo Bert akaangalia chini, akavuta hilo komeo, akaliingiza kwenye hiyo thelathini-sufuri-sita. Naye alikuwa hodari sana wa shabaha. Nami nikamwona ameilenga namna *hii*, nami nikajua angeulipua moyo wake mwaminifu moja kwa moja kupitia pande zote mbili, na risasi ya uyoga, ya kipimo cha mia moja themanini. Ndipo nikawaza, “Unawezaje kufanya hivyo, Bert? Unawezaje kuwa katili jinsi hiyo, kumwita mama kulungu huyo moja kwa moja kutoka huko na kuupiga risasi moyo wake moja kwa moja umtoke, na huku anajaribu kumtafuta mtoto wake? Unawezaje kuwa katili hivi kufanya hivyo?” Nilikuwa nikiwazia hayo. Ndipo nikamwona amemlenga *hivyo*.

189 Nami nisingeweza kuninii, nisingeweza kuangalia hilo. Lilizidi mno. Nadhani kweli mimi ni mwoga. Nikageza mgongo wangu, kisha nikawaza, “Mungu, anawezaje kufanya hivyo? Mwanadamu anawezaje kuwa katili namna hiyo, kufanya hivyo, kuupiga tu risasi moyo wa maskini mama huyo mwaminifu umtoke?”

¹⁹⁰ Sasa, yeye hakuwa akijaribu kuigiza. Hakuwa akijionyesha. Yeye alikuwa ni mama. Alimwona mwindaji huyo wakati alipoishusha bunduki hiyo chini, lakini je! alitimua mbio? La, bwana. Mtoto wake alikuwa kwenye shida, naye alikuwa akijaribu kumtafuta mtoto wake.

¹⁹¹ Ndipo nikaugauza mgongo wangu, kama nilivyosema, na kuanza. Nikasema, “Bwana Mungu, anawezaje kufanya jambo hilo?” Nikaona, na kungoja, nikangoja, bunduki haikupiga.

¹⁹² Basi nikageuka nikaangalia, nayo bunduki hiyo ilikuwa ikifanya *hivi*. Hakuweza kuishikilia tena. Akageuka, maskini macho hayo makubwa ya mji yalikuwa yamebadilika, machozi yalikuwa yakimtiririka shavuni mwake. Akaitupa bunduki kwenye tuta, na akasema, “Billy, yamenitosha. Niongoze kwa huyo Yesu unayenena habari Zake.”

¹⁹³ Moja kwa moja kwenye tuta hilo la barafu nikamwongoza kwa Kristo. Kwa nini? Aliona kitu kilicho halisi, aliona kitu cha kweli. “Wakininii... wakinyamaza hawa, mawe yatapiga kelele.” Mama huyo hakuwa akiigiza lolote. Yeye alikuwa ni mama halisi. Haidhuru kama ilikuwa ni mauti, ama chochote kile, alikuwa akiyakabili mauti moja kwa moja, akijua ya kwamba dakika yoyote ile risasi ingeulipua moyo wake wote, bali alikuwa akimtafuta mtoto wake.

¹⁹⁴ Loo, laiti tungalikuwa Wakristo kadiri huyo kulungu alivyokuwa mama! Mbona? Yeye alizaliwa mama, alizaliwa kuwa mama. Sisi tumezaliwa tupate kuliadini Neno la Mungu. Tumezaliwa kumwamini Yesu Kristo.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹⁹⁵ Ni wangapi humu ndani sasa hivi, wakiwa na mkono ulioinuliwa, wangesema, “Ndugu Branham, kwa yakini ningetaka kuwa Mkristo wa jinsi ambavyo maskini kulungu huyo alivyokuwa mama. Na—natamani moyo wangu ungalikuwa umejaa Kristo sana hata ningeweza kusimama mbele ya kitu chochote na kuwa Mkristo halisi kama tu vile huyo kulungu alivyokuwa ni mama. Mimi, hilo ndilo tukio ninalotaka?” Utauinua mkono wako? Mungu akubariki. Hilo linapendeza. Mungu akubariki. Wengi sana, kila mahali. Nina shukrani sana kwamba ungali una kitu fulani kilicho halisi ndani yako ambacho kitakufanya kuamini.

¹⁹⁶ Mnaona, vipi kama ilikuwa kwamba hukuamini? Hilo si lingekuwa ni jambo la kusikitisha, kumwona asiyeamini mahali ambapo mioyo yao ni migumu sana hata wasingeweza kuamini hata kidogo, wameangamia, wamekwisha, wamepotea, hawajui lolote kuhusu jambo hilo, hawajui ni saa ngapi mauti itabisha mlangoni? Huna budi kutoka uingie katika umilele.

¹⁹⁷ Na Yesu alisema, “Mtu asipozaliwa mara ya pili,” awe Mkristo kadiri huyo kulungu alivyokuwa mama, “kamwe hutamwona Mungu; umekwisha, haidhuru utajiunga na

makanisa mangapi.” Yeye alikuwa akizungumza na kiongozi wa dini wa siku ile, Nikodemo, mtu mwenye umri wa miaka themanini, na kumwambia ya kwamba hana budi kuzaliwa, hana budi kuwa Mkristo kama vile yule kulungu alivyokuwa ni mama pale.

¹⁹⁸ Kuna mmoja ambaye hakuinua mikono yake, ambaye kweli anajua Uwepo wa Mungu, anautambua na kusema, “Ninajua ya kwamba niko makosani”? Wakati unapotambua ya kwamba uko makosani, unautambua Uwepo wa Mungu.

¹⁹⁹ Lakini wakati hujui ya kwamba umekosea, Biblia ilisema, “U mnyonge.” Katika wakati huu, kanisa lingekuwa “nyonge, lenye mashaka, maskini, kipofu, na uchi, wala halijui.”

²⁰⁰ Wazia tu kama mwanamume ama mwanamke alikuwa barabarani, mnyonge, kipofu, maskini, mwenye mashaka, na uchi, nawe ungeweza kuwaambia kwamba walikuwa uchi, nao wangekusikiliza, lakini vipi kama wao wako uchi wala hawaamini hivyo? Hiyo ni hali mbaya jinsi gani ya akili!

²⁰¹ Vema, sasa, hiyo ndiyo hali ya kiroho iliyopo. Watu ni vipofu kiroho, wanyonge, wenye mashaka, uchi mbele za Mungu, wenye dhambi wakijaribu kujifunika nyuma ya majani ya mtini ya madhehebu fulani, wala hawajui.

²⁰² Utainua mkono wako, mtu mwingine? Mungu akubariki. Hilo ni sawa. Bwana akubariki. Kabla wewe... Labda wewe ni mgeni hapa, hujapata kumwona Mungu akifanya lolote. Lakini kabla hujaona jambo lolote, wewe, ungali unasema, “Nitalikubali juu ya msingi wa Neno. Ninajua ya kwamba aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa; Roho Mtakatifu mkuu wa Mungu yupo hapa. Ninamhisi. Ninamwamini. Nitainua mkono wangu. Mimi ni mwenye dhambi; nitaomba wokovu.”

²⁰³ Baba wa Mbinguni, wabariki hawa walioinua mikono yao juu. Tunaomba ya kwamba rehema Yako itolewe kwa wale walio—walio wenye dhambi. Hiyo ni kusema, labda wao ni wafuasi wa kanisa. Wao, hilo bado halimaanishi wao si wenye dhambi. Nao waliinua mikono yao, wanataka kuokolewa. Bwana, kulikuwako na Kitu fulani karibu nao. Walimtambua Roho Mtakatifu pale. Nao—nao walitambua ya kwamba ilikuwa ni Mungu, Naye alikuwa akinena nao, kwamba, kwamba hawakuwa na lile tukio wanalopaswa kuwa nalo, nao waliinua mikono yao.

²⁰⁴ Wewe ulisema, “Yeye atakayekuja Kwangu, sitamtupa kamwe.” Nami ninajua hiyo ni kweli. Ulisema, katika Yohana Mtakatifu 5:24, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele; hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Yeye ajaye Kwangu, nitampa Uzima wa milele, nitamfufua katika siku za mwisho.” Hizo ni ahadi Zako, Baba.

205 Ninam dai kila mmoja wao. Labda Mkristo fulani, Bwana, ambaye anajitahidi kutembea katika maisha haya, akijaribu kuishi bora zaidi, kila siku, na wao—wao wanataka tukio la—la—la mwenendo bora zaidi, waliinua mikono yao, pia. Baba, ninaomba ya kwamba utawabariki. Jalia wapate ule utoshelevu wote usiku wa leo katika Kristo, Neno lililofanyika mwili miongoni mwetu. Tujalie haya, Bwana. Ninawakabidhi Kwako, katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina.

206 Mungu awabariki. Na wakati mkiketi kimya kabisa, mnaona, kwa dakika moja; loo, jamani, nimepitisha wakati wangu kwa dakika tano sasa. Samahani, sikukusudia kuzungumza kwa muda mrefu hivyo. Nawaambieni, hebu na tungoje tu kwa dakika moja, nipeni tu dakika zingine tano, tafadhali.

207 Ni wangapi wanajua kile Mungu alichokuwa? Tunajua kile Biblia ilichosema Yeye alikuwa, na Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Na Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu mlango wa 14, kifungu cha 12, Yeye alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Si yule anayejifanya anaamini, bali, “yeye aniaminiye Mimi.” Hiyo ni kweli, ndugu zangu wahudumu? Hiyo ni kweli. Ni wangapi wasomaji wa Biblia wanaojua hiyo ni kweli? “Mbingu na nchi zitapita,” bali Maneno Yake hayawezi kushindwa. Yeye aliahidi hilo.

208 Sasa kuna, hapana shaka, wagonjwa miongoni mwenu huko mliko. Siwajui, hata kidogo. Na kuthibitisha yale niliyokuwa nikisema muda mfupi uliopita, kama Malaika wa Bwana katika siku zilizopita, siku za nyuma, zilizopita, Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Mnaweza kuona kile nilichokuwa nikizungumza habari zake, majina hayo na mengine yote yakiwa mahali pao, kanisa likiwa limekaa sawa, mnaweza kuliona? Sasa nina hakika mlisoma katikati ya mistari katika mambo ambayo sikutaja, mnaona nililomaanisha. Sasa kama ninyi watu hapa ndani, mlio wagonjwa na wahitaji, mimi ni . . .

209 Nina shughuli gani kuwa hapa? Ngingekuwa nimesimama hapa kwa sababu gani, kama mdanganyifu? Kama nilikuwa nikifanya hivyo, wakati umewadia kwangu kuninii . . . Mimi, sininii, sistahili kuishi. Mimi, afadhali nife. Mimi, afadhali nitoke niende niwe kitu kingine chochote kuliko kuwa mdanganyifu. Basi Mungu atanifanyaje? Na sijui kwamba nitaishi usiku kucha, wala wewe hujui. Lakini mdanganyifu, tunataka kuwa . . . Kuna faida gani kuwa mdanganyifu, wakati unaweza kuwa mkweli? Lakini, unaona, ni jambo geni sana kwenu.

210 Sasa, angalieni, kama ninadai ya kwamba Maandiko haya hayana budi kutimizwa, ambayo nimesoma na kuwaonyesha

katika siku hizi mbili zilizopita usiku, kile Yesu alichokuwa, kile Uwepo Wake ulicho sasa! Naye anapaswa kurudi katika siku za mwisho, tunajua hilo, kupitia mwili wa mwanadamu, na kujitangaza Mwenyewe vivyo hivyo. Sote tunajua hilo. Je! tuna habari nalo? Semeni “amina” kama ndivyo. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Sasa kwa ajili ya faraja yenu, nawaambia, nawaambia jambo hili, katika Jina Lake: Yeye yupo hapa, Mungu yeye yule aliyeshuka chini na kusema na Ibrahimu, aliyekuwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, na Sara akiwa ndani ya hema, Yeye alijua aliyokuwa akiwazia.

²¹¹ Yeye alisema jambo lile lile wakati alipokuja hapa. Aliwaangalia wasikilizaji na kujua kilichokuwa moyoni mwao. Mwanamke mmoja aligusa vazi Lake; akaangalia kote kote mpaka akampata, na kumwambia.

²¹² Bartimayo kipofu aligusa vazi Lake, wakati aliposema kwa sauti kuu, “Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu,” akisimama yadi mia mbili kutoka mahali alipopitia. Imani yake ilimsimamisha Mwana wa Mungu, barabarani, ndipo akageuka na kusema, “Mleteni hapa.”

²¹³ Maskini Zakayo juu ya mti, alijificha, kasema, kwa hiyo hakuamini Yeye alikuwa ni Nabii, yeyote. Ndipo Yesu akaja moja kwa moja, akasimama chini ya ule mti na kuangalia juu, na kusema, “Zakayo, shuka chini,” akamwita jina lake.

²¹⁴ Wakati Yesu hakuwa wakati wowote amemwona Petro, na Andrea alikuwa amemleta pale. Wakati alipomwona akija, alisema, “Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona,” alimpa jina lake, akamwambia kwamba alikuwa ni nani.

Akamwambia Nathanaeli mahali alipokuwa, yale aliyokuwa amefanya.

²¹⁵ Yule mwanamke, na hali aliyokuwamo, shida yake ilikuwa ni nini, ugonjwa wake ulikuwa ni nini.

²¹⁶ Huyu ni Mungu, enyi marafiki! Ni wangapi wanaoamini hilo kwa moyo wenu wote, waseme, “Huyo hana budi kuwa ni Mungu?”

²¹⁷ Ni wangapi wenu humu ndani mnaojua ya kwamba sijui hata jambo moja kuwahusu ninyi, inua mkono wako, useme tu, “Ninajua mtu yule hajui lolote kunihusu mimi, ninii tu—ninii tu yeye ni mwanadamu tu”? Hivyo ndivyo nilivyo, ndugu yenu tu. Nipo hapa kujaribu kuwasaidia.

²¹⁸ Lakini ninatangaza! Ni wangapi wamekisoma kitabu changu na kadhalika? Wewe, unajua, unaamini hilo, ni Kweli? Hizi ni siku za mwisho. Na sasa Bwana Yesu na atusaidie.

²¹⁹ Na kama Yeye atakuja usiku wa leo... Na hebu mmoja wenu asisogee. Kaeni moja kwa moja vitini mwenu mahali mlipo, na mwamini, Naye Bwana Yesu atakuja usiku wa leo na kuthibitisha mambo haya ambayo amesema, mambo haya

ambayo aliahidi. Kama atayathibitisha kuwa ni Kweli, je! mtamwamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Aminini!

220 Baba wa Mbinguni, sasa nimezungumza juu Yako, kile ulichokuwa, kile ulicho, sasa naomba ujitokeze jukwaani. Na hao watu wanaoketi huko katika wasikilizaji, wageni kabisa, je! utajitambulisha kwetu usiku wa leo, Bwana, tupate kujua na kutambua ya kwamba Maandiko haya yametimizwa, kwamba “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele”? Basi kama tunaishi katika siku za mwisho, kama Yeye alivyosema ya kwamba angejifunua Mwenyewe katika siku za mwisho, kama alivyofanya kule Sodoma kabla ya yule mwana aliyeahidiwa kuja kwa Ibrahimu, vema, uzao wa kifalme wa Ibrahimu ambao unamtazamia Mwana wa kifalme, jambo lile lile lingetukia. Na angalia hata na mahali penyewe, wakati, majina, na kila kitu ni kikamilifu kabisa, Baba. Tusaidie, tunaomba, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

221 Sasa nawatakeni mwombe, kila mmoja wenu. Shida yoyote, mwombeni tu. Sasa Yeye ni Kuhani Mkuu.

222 Jambo lingine, ni wahudumu wangapi walio humu jengoni, inueni mikono yenu, kila mahali? Nadhani kuna thelathini ama arobaini. Sasa ni wangapi wenu mnaojua jambo hili, ya kwamba Kitabu cha Waebrania, Agano Jipya, kinatwambia kwamba sasa hivi “Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo ya udhaifu wetu”? Mngeweza kuinua mikono yenu na kusema, “Ninajua ni Kweli. Biblia inasema hivyo”? Hiyo ni kweli. Vema.

223 Basi kama Yeye ni Kuhani Mkuu, Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Basi kama ungemgusa usiku wa leo, Yeye angetenda kama vile alivyofanya kule nyuma. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kama alivyofanya jana!

224 Vema, wakati mwanamke yule alipoligusa vazi Lake. Mnasema, “Loo, laiti ningeweza!” Imani yako ndiyo inayoligusa. Kimwili, Yeye hakuhisi. Ilikuwa ni imani ya mwanamke huyo, ambayo ililigusa vazi hilo. Imani yako inaweza kumgusa sasa. Unaamini hilo?

225 Basi kama Neno la Mungu linadhihirishwa, Yeye atafunua jambo lilo hilo na kuonyesha jambo lilo hilo. Mnaamini hilo kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema, sasa mtumainini tu Yeye, mwaminini. Msitie shaka. Bali iweni na imani kwa Mungu, ya kwamba atalifanya. Mtu fulani upande *huu*, omba tu na uamini tu kwa moyo wako wote, halafu mtu fulani upande *huu*. Na kama Mungu atajalia mtu mmoja ama wawili mnaowajua, ambao hauwezi kukosea, ni wangapi wenu wataamini basi ya kwamba tunautambua Uwepo Wake? [“Amina.”] Basi hilo tu ndilo linalohitajika. Hilo tu ndilo linalohitajika.

226 Mama anayeketi moja kwa moja pale, akiniangalia pale, akiugua ugonjwa wa moyo. Je! unaamini Mungu atakuponya huo moyo, akufanye mzima? Una ugonjwa wa moyo. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Je! hatufahamiani, sikujui? Lakini hiyo ni kweli, vema, wewe, huyo mama, mama mwenye mvi anayeketi hapo. Vema.

227 Mama aliye na ya kijanikibichi, uliunua mkono wako hapo, ya kwamba wewe—wewe. . . Shida yako ni yabisi kavu. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, na yabisi kavu? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaona? Vema. Unaona? Ilitokea tu aliinua. . . Sasa Kitu fulani kilikushukia, sivyo? Unaona, ile Nuru. Ni wangapi waliopata kuona picha ya ile Nuru? Ilining'inia, pale pale juu ya yule mwanamke. Mara moja hisi tamu sana ilikuja juu yako. Hiyo ndiyo iliyoisababisha, unaona. Mungu alikubariki, akakuponya, akakupa afya. Unaamini hilo?

228 Je! unaamini Yeye anajua shida yako? Yeye tu Ndiye anayeweza kukuponya. Ni kivuli cheusi, kifafa. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, ewe msichana. Wazia tofauti kidogo kuliko ulivyofanya dakika chache zilizopita, sivyo? Uliona wakati niliposimamisha wito huo, kufanya hivyo? Hiyo ndiyo sababu yake, ilikuwa ni kwa ajili yako. Sasa kama utaamini hilo kwa moyo wako wote, basi vipindi hivyo vya kifafa vitakuacha. Utalikubali na kuamini kwa moyo wako wote? Mungu akubariki. Nenda zako, amini hilo.

229 Mama huyu anayeketi papa hapa, akiugua ugonjwa wa tumbo, unaamini ya kwamba Mungu atakupa afya? Papa hapa mwisho, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, atakuponya ugonjwa wa tumbo? Unaamini, unalikubali hilo? Vema. Mungu akubariki.

230 Mimi sifahamiani kabisa na mwanamke huyu, simjui. Yeye ni mwanamke tu anayeketi hapo, lakini Mungu anamjua. Unaamini kwa moyo wako wote sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, iweni tu na imani.

231 Mama anayeketi papa hapa mwisho, anaugua ugonjwa wa kibofu nyongo. Ana vijiwe nyongo, ini, linakusumbua. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako; hatufahamiani kabisa, kama hiyo ni kweli. Unaona?

232 Mama anayeketi papo hapo karibu na wewe, anaugua, pia. Mnaiona, hivi hamwezi kuona hiyo Nuru juu ya mwanamke yule? Mama huyo ana ugonjwa wa figo, Hiyo ni kweli. Ana sumu damuni katika mafigo yake. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mama huyo aliyekugusa wakati huo, anaugua ugonjwa wa mateso ya—ya wasiwasi. Nyote ni wageni, hamtoki hapa. Hiyo ni kweli, sivyo? Mmetoka Iowa. Mmetoka katika jiji la Des Moines. Hiyo ni kweli, sivyo? Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia jina lako ni nani, kama alivyomwambia Petro? Kama

utaamini kwa moyo wako wote! Jina lako ni Bibi Wolff. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema, rudi umeponywa sasa, Yesu Kristo anakuponya.

²³³ Je! mnautambua Uwepo Wake, mnajua Yeye yupo hapa? Basi nawaomba mwekeane mikono sasa, wakati Roho Mtakatifu akiwa juu yenu. Huyu ni Roho Mtakatifu juu yenu. Sasa kila mmoja wenu anaweza kuponywa sasa kama mtaamini tu. Mnaamini kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²³⁴ Baba wa Mbinguni, hakuna kitu kilichosalia sasa ila imani. Sasa tunakataa giza lote. Wakati uamsho, kama nilivyosema hapo mwanzo, mawimbi yalikuja juu ya maji kuyatibua juu chini, ku—ku—kuondoa kutokuamini kutoka kwake; sasa wakati Roho Mtakatifu anapopepea hapa huku na huku katika watu hapa, jalia kutokuamini kote kuondolewe, na jalia uwepo wa Mwenyezi Mungu umweke kila anayeteseka huru usiku wa leo.

²³⁵ Ninamkemea ibilisi. Shetani, wewe si kitu ila mdanganyifu, nawe umefichuliwa papa hapa miongoni mwa watu, kwa ushuhuda wa Kimaandiko wa Yesu aliyefufuka aliye hai. Ninakuapisha, kwa Mungu aliye hai, toka ndani ya watu hawa na uwaache waende, kwa utukufu wa Mungu.

²³⁶ Wote mnaoukubali uponyaji wenu, simameni kwa miguu yenu sasa na msemi, “Ninaamini. Haidhuru ni jambo gani linalotukia, inachukua muda gani, bado ninajua nitakuwa mzima. Ninaukubali, kwa moyo wangu wote.”

²³⁷ Inueni mikono yenu sasa. “Asante, Bwana.” Bwana asifiwe. Hiyo ni kweli, mpeni sifa. Sasa inueni tu mikono yenu na mumsifu kwa ajili ya uponyaji wenu, jinsi mnavyofanya makanisani mwenu. Ndugu . . .



UWEPO WA MUNGU USIOTAMBULIWA SWA64-0618

(The Presence Of God Unrecognized)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 18 Juni, 1964, katika Ukumbi wa Manispaa huko Topeka, Kansas, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org